# Nipashe

Jumamosi Septemba 5, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580329

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710





**Nipashe Jumapili linarudi tena mtaani**

Usikose nakala yako ya Nipashe Jumapili hii kwa habari motomoto za kisiasa, kijamii, burudani na safu maarufu ya 'Maisha ndivyo yalivyo' 'Madongo ya Mgaga-gigikoko' na 'Fikra mbadala'. Watoto nao hawakuachwa nyuma, bila kusahau mapishi, michezo, hadithi, mitindo, ka-tuni na muziki wa enzi zilee...




## Lissu aahidi kuwasamehe mahabusu wa muda mrefu

UKURASA 3

# Ubwabwa wa Rungwe wapigwa marufuku

**TAKUKURU** yamuonya, mwenyewe asisitiza utakuwapo leo kwenye uzinduzi wa kampeni...*Endelea ukurasa 2*



Mgombea Urais wa CCM, John Magufuli

## JPM atamba kutengeneza ajira maelfu

UKURASA 2



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NCBA Tanzania Ltd, Margaret Karume (kushoto), akijadiliana jambo na viongozi waandamizi wa IPP Media, (kutoka kulia) Mkurugenzi wa IPP, Joyce Luhanga, Meneja wa Kiwanda cha Uchapishaji cha Kampuni ya The Guardian Ltd (TGL), inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, Balasubramaniyan Venkadachalam, Meneja wa Sheria na Raslimali Watu wa TGL, Emmanuel Matondo na Mhariri Mtendaji wa gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe, alipotembelea chumba cha habari cha kampuni hiyo, Mikocheni, jijini Dar es Salaam jana. **Picha zaidi Uk. 7**. PICHA: JOHN BADI

## DPP AFUTA MASHTAKA KUWANUSURU MAMIA JELA

UKURASA 5

**MICHEZO** YANGA YATOA SABABU KUVUNA TATU ZA PRISONS UK.24

**MAONI, KATUNI UK.6**


**Fursa kwa Wagombea! 2020**

VOTE

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini

Je ungependa kukishukuru chama chako ?

Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?

Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe MWANGA WA JAMII

Wasiliana nasi

Simu: 0686 101335,

Barua pepe: advertise@guardian.co.tz

VOTE

# NCCR kuanza kampeni rasmi

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha NCCR-Mageuzi leo kinazindua kampeni zake katika viwanja vya Mbagala Zakhem, jijini Dar es Salaam, huku kikijinasibu kutangaza sera bora kwa wananchi nchi nzima.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkuu wa Mawasiliano na Uenezi kwa Umma wa chama hicho, Edward Simbeye, alisema ratiba ya uzinduzi huo itaanza saa 2:00 asubuhi mpaka saa 12:00 jioni.

Simbeye alisema tukio hilo litaambatana na uzinduzi wa ilani ya chama hicho.

"Ni tukio ambalo litakuwa na mambo mengi siku hiyo ya kesho (leo) kwa sababu litaambatana na uzinduzi wa ilani ya chama ambayo baada ya hapo tutaisambaza katika vyombo vya habari vyote na mitandao ili kila mmoja aipate," alisema Simbeye.

"Kwa hiyo hatutakuwa na muda wa kupoteza, wagombea wetu watatoka moja kwa moja hadi viwanja vya Zakhem na hawatapitia mahali popote ili kuokoa muda," aliongeza.

Alisema baada ya uzinduzi, kesho wataendelea na kampeni katika Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam na Jumatatu watakuwa Makete mkoani Njombe kuendelea na kampeni hizo.

"Wagombea wetu watakwenda nchi nzima kufanya kampeni kulingana na ratiba ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) itakavyokuwa inapangwa, kwa hiyo wananchi wakae mkao wa kula kusikiliza sera za NCCR-Mageuzi ambazo zinajibu changamoto ambazo wamekuwa wakilia kwa muda mrefu," alisema Simbeye.

Chama hicho ambacho kinajinasibu kwa kauli mbiu ya 'Utu Itikadi Yetu', mgombea wake wa nafasi ya urais kwa upande wa Jamhuri ya Muungano ni Yeremia Maganja na mgombea wake mwenza ni Haji Khamis.

# Ubwabwa wa Rungwe wapigwa marufuku

**Na Thobias Mwanakatwe**

WAKATI mgombea urais kupitia Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA), Hashimu Rungwe, akitarajia kuzindua kampeni zake leo, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imemwonya kuhusu ahadi yake ya kuwapa ubwabwa wananchi watakaokwenda kwenye mkutano wake.

Huku taasisi hiyo ikisema kugawa chakula hicho ni kosa kisheria na ni rushwa, mgombea huyo amesisitiza kuwa wananchi wajitokeze kwa wingi na kwamba ubwabwa utakuwapo.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Ilala, Christopher Myava, alitoa onyo hilo jana wakati akihojiwa na kituo kimoja cha redio jijini Dar es Salaam.

Myava alisema Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya mwaka 2010 inapiga marufuku kwa mgombea kutoa vitu kama chakula kushawishi wapigakura ili wamchague.

"Kwa mujibu wa sheria, kutoa chakula ni kosa kwa sababu huo ni ushawishi kwa kuwapa chakula ili wakupigie kura. Kwa nini afanye haya katika kipindi hiki cha uchaguzi kwani kuna shughuli ngapi ambazo zinafanyika? Mikutano mingapi ambayo inafanyika watu hawaweki 'bufee'?" Alihoji.

Myava alisema kipindi hiki kinachotakiwa kufanywa na mgombea ni kunadi sera zake ili kuomba ridhaa ya wananchi kumchagua na si kushawishi kwa kutoa rushwa.

"Unapotoa chakula kipindi hiki cha kampeni kabla hata hujachaguliwa, huo ni ushawishi kwa mujibu wa sheria hizi. Anachotakiwa kukifanya mgombea ni kunadi sera na si kushawishi watu kutokana na chakula anachokitoa," alisisitiza Myava.

Rungwe akizungumza juzi na gazeti hili alisema leo atazindua kampeni zake eneo la Bakhresa, Manzese jijini Dar es Salaam kuanzia saa 9:00 alasiri na kuwaomba wananchi wahudhurie kwa wingi kwa sababu kutakuwa na ubwabwa ambao watagawiwa bure.

Rungwe amekuwa akilisisitiza suala la kutoa ubwabwa kwenye mikutano yake ya kampeni kiasi cha kuwavutia wananchi ambao wamekuwa wakitoa maoni yao kwenye mitandao ya kijamii kusubiri mikutano yake ianze.

**MSIMAMO WA RUNGWE**

Rungwe alipoulizwa msimamo wake baada ya tamko hilo la TAKUKURU, alisema ubwabwa utakuwapo kama kawaida na kudai kuwa kufanya hivyo si rushwa.

"Hiyo siyo rushwa nitatoa ubwabwa kama kawaida kwenye mkutano. TAKUKURU wajiandae kupelekana mahakamani," alisema Rungwe alipohojiwa na Nipashe.

Rungwe ambaye amekuwa mgombea anayetoa burudani kutokana na matamko yake, juzi alitoa mpya baada ya kueleza kuwa kama wananchi watampa ridhaa kuwa Rais, miongoni mwa mambo atakayofanya ni pamoja na kuuza ndege na magari yote yanayotumiwa na viongozi waandamizi wa serikali wakiwamo mawaziri na wakuu wa mikoa.



Mgombea urais wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais John Magufuli, akihutubia maelfu ya wananchi katika mkutano wake wa hadhara wa kampeni mjini Bariadi, mkoani Simiyu jana. **PICHA: IKULU**

# JPM atamba kuzalisha ajira mamilioni

**Na Gwamaka Alipipi,** SIMIYU

MGOMBEA urais kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais John Magufuli, ametamba kutengeneza ajira lukuki katika kipindi cha miaka mitano huku akisema atafanya hivyo kwa zaidi endapo atachaguliwa tena.

Amesema katika kuanza utekelezaji wa azma hiyo, akizungumza na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, kutangaza ajira 13,000 za walimu wa shule za msingi na sekondari muda wowote kuanzia sasa.

Rais Magufuli alitoa ahadi hiyo jana mjini hapa wakati akizungumza na maelfu ya wananchi na wanachama wa CCM walioijitokeza katika Uwanja wa Shule ya Msingi Somanda, kumsikiliza akinadi sera.

Alisema kwa kipindi cha miaka mitano ya utawala wake kuanzia mwaka 2015, ametengeneza ajira milioni sita katika sekta rasmi na isizo rasmi, hivyo ameweka mikakati mingine ya kuhakikisha Watanzania wengi wanapata ajira katika viwanda na ujenzi wa reli ya kisasa.

"Ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma umeshatoa ajira 10,000 na tunatarajia kuajiri Watanzania wengi zaidi katika mradi huo. Ajira ni mipango," alisema na kuongeza:

"Hiyo reli itakapojengwa kuanzia Morogoro hadi Makutupora watakaojenga ni Watanzania, hivyo wataajiriwa. Tutajenga barabara nyingi na watakaojenga ni Watanzania, tutajenga hospitali napo Watanzania wataajiriwa, hivyo ajira nyingi zinakuja."

Rais Magufuli alisema ilani ya CCM inaeleza kuwa zitatengenezwa ajira milioni nane kutoka sekta rasmi na isiyo rasmi.

"Ndugu zangu wa Bariadi, ninaomba kura ili niwe Rais kwa miaka mitano ijayo na nitekeleze hayo yote. Kwa miaka mitano tumeajiri Watanzania wengi, tuliajiri madaktari zaidi ya 1,000, watumishi wa afya zaidi ya 14,000, ajira zaidi ya milioni sita zilitengeneza," alisema.

**MAFANIKIO SIMIYU**

Kuhusu mafanikio ya Mkoa wa Simiyu kwa miaka mitano, mgombea huyo alisema serikali ilifanikiwa kujenga hospitali ya rufani ya mkoa na za wilaya za Bariadi na Itilima.

Sambamba na hospitali hizo, pia alisema vimejengwa vituo vya afya vitatu na zahanati 14 pamoja na kununua vifaa tiba na dawa kwa thamani ya Sh. bilioni 15.

"Tumeboresha huduma za afya. Zaidi ya Sh. bilioni 32.3 zimetumika katika sekta ya afya Simiyu. Vifo vya watoto vimepungua kutoka watoto 392 hadi 100 kwenye kila kaya 100,000," alisema.

Kuhusu elimu, Magufuli alisema zaidi ya Sh. bilioni 73.8 zimetumika mkoani humo kununua madawati 88,185, ujenzi wa nyumba za walimu 28, ujenzi wa mabweni 17, walimu 1,116 wameajiriwa.

Akizungumzia ujenzi wa barabara, alisema kilomita 117.1 za barabara ya lami zimejengwa kwa thamani ya Sh. bilioni 2016.2 na barabara za changarawe zenye urefu wa kilomita 293.

"Tumejenga barabara kutoka Bariadi hadi Maswa (km 112), Bariadi Mjini (km 17.8), tumeweka taa za barabarani, tumejenga stendi pamoja na maegesho ya magari, ujenzi wa daraja la Sibiti," alisema.

Kuhusu nishati, Magufuli alisema serikali imetumia Sh. bilioni 81.1 kwa ajili ya kupeleka umeme katika vijiji 229 mkoani humo.

Kadhalika, Magufuli aliwaahidi wakulima wa pamba kuwa kutajengwa kiwanda cha kuchakata zao hilo na kwamba nguo zitakuwa zinatengenezwa hapa nchini kisha kusafirishwa nje.

# Magufuli atoboa Chenge alivyomsaidia 200,000/-

**Na Gwamaka Alipipi,** BARIADI

MGOMBEA wa urais kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, amefichua alivyopewa msaada wa Sh. 200,000 mwaka 1995 na aliyekuwa Mbunge wa Bariadi, Andrew Chenge, kwa ajili ya matibabu ya mkewe, Mama Janeth Magufuli.

Akisimulia tukio hilo wakati wa mkutano wa kampeni mkoani Simiyu jana, Dk. Magufuli alisema: "Ninawashukuru sana hawa wabunge waliomaliza muda wao. Katika siasa, kuna miaka 10, lakini nimezungumza maeneo mengi kazi ziko nyingi.

"Chenge ni kaka yangu kweli kweli, wala siyo uongo. Nilipoingia bungeni kwa mara ya kwanza mwaka 1995, mke wangu alikuwa mjamzito.

"Aliyenisaidia hela ya kwenda hospitali Sh. 200,000, alitoa Chenge. Ndiyo maana ninasema ni kaka yangu. Sasa ni zamu ya Mhandisi Mfungo, Chenge 'emilimo eleminge'," Dk. Magufuli alisema kwa lugha ya Kisukuma akimaanisha kazi ni nyingi.

Katika mkutano huo, Dk. Magufuli alimkaribisha Chenge kusalimia wananchi na wanachama wa CCM waliojitokeza katika kampeni hizo, Mwanasheria Mkuu huyo wa zamani wa Serikali akimpongeza kiongozi huyo wa nchi kwa kuitenda haki Bariadi katika miaka mitano iliyopita ya uongozi wake.

Alisema kuwa Dk. Magufuli ameitendea haki Tanzania na kupita kwake kuomba kura kuelekea uchaguzi mkuu wa Oktoba 28 ni kutekeleza tu matakwa ya kikatiba, lakini ameshinda.

"Dk. Magufuli ninakushukuru sana kwa kuzungumza vizuri ile historia ya mwaka 1995 ya kutoa fedha kwa ajili ya mama Janeth ambaye naye ana upendo mkubwa sana. Sikutegemea kama historia ungeisema vizuri mbele ya watu," alisema Chenge.

Alifafanua kwamba mwaka 2005 aliipogombea ubunge wa Bariadi, alifanikiwa kulikomboa jimbo hilo kutoka upinzani.

"Tutahakikisha safari hii kura zinakuwa za kutosha sana. Nimhakikishie kijana wetu (mgombea ubunge), mimi Andrew Chenge nitafanya kazi ya uhakika.

"Tutatembea bega kwa bega kuhakikisha tunapata kura za kutosha, tutakwenda kata zote 31 katika jimbo letu ingawa tayari madiwani wa kata saba wamepita bila kupingwa, lakini tutakwenda kutafuta kura kwa ajili yako, mbunge na madiwani," aliahidi.

# Lissu aahidi kuwasamehe mahabusu wa muda mrefu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA



MGOMBEA urais kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu (pichani), ameahidi kusamehe mahabusu wanaoshikiliwa kwa muda mrefu katika magereza mbalimbali nchini, ikiwa atafanikiwa kushinda kiti hicho katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 28 mwaka huu.

Lissu alitoa ahadi hiyo jana alipohutubia wananchi waliojitokeza kumsikiliza katika uzinduzi wa kampeni za chama hicho Kanda ya Kati uliofanyika jijini.

Mtaalamu huyo wa sheria aliahidi kuwa endapo akifanikiwa kushika nafasi hiyo ya juu ya uongozi nchini, atahakikisha anamaliza msongamano wa mahabusu magerezani ndani ya miezi mitatu ya mwanzo madarakani.

Alisema hilo litafanikiwa kwa kufanya marekebisho kwenye sheria za nchi ili kuongeza idadi ya makosa yote yanayostahili kuwa na dhamana.

"Wapo watu wanashikiliwa mahabusu kwa miaka mingi, wameshikiliwa wapo ndani bila kupewa dhamana. Sasa mimi katika utawala wangu mambo hayo ya uonevu hayatakuwapo na tutafanya kwa haki," aliahidi.

Lissu pia aliendelea kusisitiza kuwa katika utawala wake atafanya mabadiliko makubwa katika sheria zote za makosa ya jinai na hakutakuwa na kosa ambalo halina dhamana.

Alisema sekta ya afya inakabiliwa na kero mbalimbali, ambazo akichaguliwa atahakikishia anazitatua kwa mbinu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuweka utaratibu wa bima ya afya kwa wananchi wote.

"Jana (juzi) nilikuwa Tabora, nikaambiwa kuwa mama akijifungua mtoto wa kiume anatakiwa kulipa kodi Sh. 50,000 na akijifungua mtoto wa kike Sh. 40,000. Hii sisi tutaikomesha, tukishaanzisha mfumo huu wa bima kwa wote, utawasaidia wananchi katika masuala ya afya," alitamba.

Lissu alisema kuwa katika Jiji la Dodoma, atahakikisha anakomesha vitendo vya bomoabomoa ambavyo alidai vinafanywa kwa kisingizio cha kupisha shughuli za maendeleo bila kuwalipa wananchi fidia.

Mgombea huyo pia alisema kuwa akichaguliwa, atarekebisha utaratibu wa utoaji wa mafao kwa wafanyakazi ili serikali yake itimize kwa vitendo kile alichokiita uhuru na haki kwa wananchi, likiwamo kundi hilo la wafanyakazi.

"Hadi leo, serikali ya awamu ya tano inamaliza muda wake haijawahi kuongeza mishahara kwa wafanyakazi, mimi nitahakikisha ninafuata matakwa ya sheria na kuwapatia haki yao ya kimsingi," alisema.

Awali, Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Kati, Lazaro Nyalandu, alisema wamewasilisha rufani kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) za majimbo 15 na kata 209 walizodai kutotendwa haki kwenye kanda hiyo. Mgombea Mwenza, Salum Mwalimu aliwaomba Watanzania kutumia siku tatu kuanzia jana kuiombea NEC, ili itoe uamuzi wa haki kwenye rufani zote 557 zilizokatwa nchi nzima.


CHAMA CHA WALIMU TANZANIA C.W.T WAJIBU NA HAKI

## CHAMA CHA WALIMU TANZANIA (CWT)

## NAFASI ZA KAZI

Chama cha Walimu Tanzania ni Chama cha Wafanyakazi kutoka kada ya Ualimu ambacho shughuli zake zipo Tanzania Bara tu. Chama kimesajiliwa kwa Namba 004 chini ya Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Namba 6 ya mwaka 2004 na kinaajiri Wafanyakazi kwa ajira ya kudumu ambao wapo katika kila mkoa. Ili kuboresha huduma bora kwa wanachama, zoezi la kuajiri kadri ya uhitaji halikwepeki. Hivyo Chama cha Walimu Tanzania kinahitaji kupata walimu wenye sifa na moyo wa kukitumikia kadri ya taaluma zao kwa nafasi ya Katibu wa Wilaya Tanzania.

**1. KATIBU WA WILAYA – NAFASI 12**

**(a) Majukumu ya kazi**
- Mtendaji Mkuu wa shughuli za Chama za kila siku katika ngazi ya Wilaya.
- Mtetezi Mkuu wa haki na wajibu wa wanachama ndani ya Wilaya.
- Mtetezi na msimamizi wa taaluma na utaalamu wa ualimu pamoja na elimu bora kwa wote.

**(b) Sifa za mwombaji**
- Awe ni mwalimu wa cheti cha daraja la IIIA na kuendelea.
- Awe na uelewa, ujuzi na uzoefu wa Chama na masuala ya walimu na elimu nchini.
- Awe mwalimu aliyeajiriwa na Serikali, mwenye namba ya utambulisho wa ajira (TSC Namba).
- Awe mwanachama kamili wa CWT hadi sasa na aliyechangia miezi kumi na mbili (12) mfululizo ada ya uanachama hadi tarehe ya tangazo hili.
- Awe ni mwenye tabia na mwenendo unaokubalika katika maadili ya taaluma na ualimu.
- Awe ni mwenye uwezo wa kujenga na kuendeleza mahusiano mema kati yake na wanachama, viongozi wa Chama, waajiri na wadau wa elimu.

**(c) Mshahara**
Mshahara utatolewa kwa mujibu wa Kanuni zinazotawala utumishi ndani ya CWT.

**(d) Namna ya kutuma maombi**
Maombi yatawasilishwa na mwombaji kwenye ofisi ya CWT ya Wilaya yake anapofanyia kazi. Barua ya maombi iambatane na vivuli vya vyeti vya masomo, stakabadhi ya mshahara (salary slip) wa mwisho na kitambulisho cha uanachama wa CWT pamoja na barua ya ajira.

(e) Mwombaji atapatiwa fomu maalum na Katibu wa Wilaya na atajaza taarifa zake na kuambatisha na barua yake ya maombi.

**(f) Mwisho wa kupokea maombi**
Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 21 Septemba, 2020 saa 10.00 Jioni.

**Imetolewa na:**

**Mwl. Deus G. Seif**
**KATIBU MKUU – CWT.**
**05.09.2020**

KATIBU MKUU CHAMA CHA WALIMU TANZANIA (CWT) MAKAO MAKUU - DODOMA

215887502

# Mgombea ajinadi kuboresha elimu

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MGOMBEA ubunge Jimbo la Kibaha Mjini kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Michael Mtally, amesema endapo wananchi watamchagua kuwa mwakilishi wao, atasimamia bajeti ya miundombinu ya elimu.

Mtally aliyasema hayo, juzi wakati wa uzinduzi wa kampeni za ubunge katika jimbo hilo zilizofanyika katika viwanja vya Bamba, kata ya Kongowe.

Alisema endapo wananchi watampa ridhaa ya kuwa mbunge katika kipindi cha miaka mitano, atahakikisha bajeti ya elimu katika Halmashauri ya Mji Kibaha inaboreshwa ili kuwa na miundombinu ya kutosha pamoja na vitabu kwa wanafunzi.

Pia alisema iwapo atachaguliwa, atasimamia ujenzi wa vituo vya afya vyenye hadhi ya kuwa na madaktari bingwa watakaokuwa wakitoa huduma kwa wananchi ambao kwa sasa inadaiwa wanatumia gharama kuwafuata nje ya halmashauri hiyo.

"Tutakuwa na utaratibu wa kuwapima wazee na matibabu watakuwa wanapata bure, lengo letu kusogeza huduma karibu na wananchi na wazee wasitozwe gharama. CHADEMA tunaahidi tutakuwa na maboresho makubwa katika sekta zote," alisema.

Akizindua kampeni hizo, Katibu wa CHADEMA Kanda ya Pwani, Hemedy Ally, alisema baada ya uchaguzi na chama hicho kuchaguliwa, siku 100 za mwanzo watahakikisha wanarudisha mchakato wa katiba mpya.

Aidha, alisema, chama hicho kimedhamiria endapo kitapata ridhaa ya kuongoza wataboresha mfumo wa uchumi ikiwa ni pamoja na kupunguza utitiri wa kodi kwa wafanyabiashara. Mgombea udiwani Kata ya Visiga, Deogratius Kweka, alisema endapo chama hicho kitapewa ridhaa ya kuongoza katika kata hiyo watahakikisha vijana wanapata ajira kwenye wiwanda vilivyopo ndani ya kata hiyo.

# Ajitoa kugombea ubunge kumuunga JPM

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MGOMBEA ubunge wa Hai mkoani Kilimanjaro kwa tiketi ya Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA), Ibrahim Simbo, ametangaza kujitoa katika kinyang'anyiro hicho kwa kile alichodai kumuunga mkono mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli.

Simbo alitangaza uamuzi huo juzi mbele ya waandishi wa habari, akidai kuwa ameona atajichosha bure kushindana na kutumia nguvu nyingi ilhali ana nafasi nzuri ya kumuunga mkono mgombea urais kwa tiketi ya CCM kwa kuwa kazi zake zinaonekana waziwazi.

Wagombea ubunge wanaoendelea na kampeni zao katika Jimbo la Hai ni Saashisha Mafuwe (CCM), Mbarouk Mhina (ACT-Wazalendo) na Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe.

"Kuanzia leo (juzi), nimesitisha zoezi lote na nitaunga mkono chama kinachoongozwa na Rais John Magufuli. Nina sababu za msingi, nimeona ninajichosha kutokana na mambo anayoyafanya Rais Magufuli yanaonekana kwenye jamii.

"Kwa hiyo, kwa ridhaa yangu kutoka moyoni, nitaunga mkono chama kinachoongoza serikali. Hata mwaka 2010, niligombea ubunge wa Hai, lakini kitu ninachokiona tofauti mpaka nikahama, niliona kwamba jamii yenyewe imekubali na mimi ninaangalia mbali sana.

Hata kwa nchi za wenzetu zilizoendelea, huwa wanafanya siasa za aina hii.

"Mimi nilichukua fomu ya kugombea ubunge ili kuleta changamoto, lakini baadaye nikagundua siuwezi muziki wa John Magufuli na chama chake. Ninatoa rai kwa vyama vingine, vingekuwa makini, vingemuunga mkono Rais Magufuli," alisema.

Simbo aliongeza kuwa aliamua kuchukua uamuzi wa kujitoa baada kuangalia ilani za uchaguzi za vyama vyote vya siasa vinavyoshiriki uchaguzi huo na kubaini Rais Magufuli kwa kutumia ilani ya chama chake na ahadi ambazo yeye (Simbo) alizozitoa mwaka 2015 na sasa zinatekelezeka.

"(Dk. Magufuli) alinifurahisha juzi, alisema kwamba kuna vitu atavifanya ndani ya miaka mitano na vitaisha ndani ya miaka mitatu. Na kwa sababu kazi yake inaonekana na anafanya kazi vizuri na matunda tumeyaona, nina imani ataendelea hivyo hivyo na ninawaomba wananchi tumuunge mkono," alisema.



Mratibu wa kifua kikuu na ukoma Wilaya ya Tunduru, mkoani Ruvuma, Dk. Mkasange Kihongole (mbele), akiwa na baadhi ya wataalamu na viongozi wa kijiji cha Majala, wilayani humo, walipokwenda katika kambi mojawapo ya wafugaji umbali wa km 20, kwa ajili ya kutoa elimu na uchunguzi wa ugonjwa wa kifua kikuu hasa baada ya kubainika kwamba jamii ya wafugaji ni kati ya makundi yaliyopo katika hatari ya kupata TB kutokana na kunywa maziwa yasiochemshwa vizuri. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Majaliwa asema CCM haikurupuki

**Na Mwandishi Wetu**

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema chama hicho hakikurupuki katika kuiwekea malengo serikali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya wananchi.

Amesema CCM imekuwa ikiielekeza serikali kutekeleza shughuli za maendeleo kupitia ilani ya uchaguzi ambayo imesheheni mambo yote ikiwamo miradi mbalimbali kama vile ya afya, maji, elimu na miundombinu.

Majaliwa alisema hayo juzi alipohutubia mkutano wa kampeni uliofanyika katika Uwanja wa Polisi wilayani Longido mkoani Arusha wakati akimwombea kura Rais John Magufuli na mgombea ubunge wa Jimbo la Longido, Dk. Stephen Kiruswa.

Alisema ilani ya uchaguzi ya CCM ya 2015-2020 imetekelezwa kwa mafanikio makubwa na serikali ya awamu ya tano chini ya Rais Magufuli na sasa imeandaa ilani nyingine ya 2020-2025 nayo imeweka msisitizo katika masuala mbalimbali ikiwamo uboreshaji wa huduma za jamii.

Pia alisema msisitizo mwingine uliowekwa katika ilani hiyo ni kuielekeza serikali iendelee kudumisha amani na utulivu, na kukuza uchumi. Aliwasihi wananchi kuhakikisha wanampigia kura nyingi Rais Magufuli ili aendeleze kazi kubwa aliyoanza ya kuwaletea wananchi maendeleo.

Kuhusu mifugo, Majaliwa alisema sekta hiyo ni muhimu katika ukuaji wa uchumi, hivyo serikali itaendelea kuimarisha ufugaji wa kisasa na tayari kiwanda kikubwa cha kuchakata bidhaa za mifugo kimejengwa Namanga, wilayani Longido.

Alisema kiwanda hicho kina uwezo wa kuchakata ng'ombe 300 hadi 500 kwa siku, mbuzi na kondoo 3,000 hadi 4,000 kwa siku na kinatarajiwa kutoa ajira za moja kwa moja 300. Kiwanda hicho kinatarajiwa kuanza uzalishaji baadaye mwezi huu na kuwataka wana Longido kuendelea kuiamini CCM.

"Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita 2015 hadi 2020 Chama Cha Mapinduzi kilijielekeza katika kuhakikisha sekta ya ufugaji inaimarishwa ili kuwawezesha wananchi kunufaika na ukuaji wa sekta hiyo na mafanikio tumeyaona," alisema.

Mkutano huo ulihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa CCM wa Mkoa wa Arusha na Wilaya ya Longido, wagombea wa ubunge kwa tiketi ya CCM wa majimbo yote ya mkoa wa Arusha na wagombea wa udiwani wa kata 18 za Wilaya ya Longido ambao wote wamepita bila kupingwa.

HABARI KITAIFA




Mkurugenzi wa Ubunifu na Ujasiriamali wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. Ambrose Itika (kushoto), akizungumza katika hafla ya kusaini makubaliano kati ya kampuni ya Empower Ltd na chuo hicho, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kusaidia wanafunzi katika masuala ya ujasiriamali na ubunifu. Katikati ni Naibu Makamu Mkuu wa chuo (Utafiti), Prof. Bernadeta Killian na Mkurugenzi Mtendaji na mwasisi wa kampuni hiyo, Miranda Naiman. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Washtakiwa 147 wafutiwa mashtaka

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WASHTAKIWA 147 mkaoni Shinyanga wamefutiwa mashtaka yaliyokuwa yakiwakabili na kuachiwa huru na Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Biswalo Mganga, huku wengi wao wakiwa ni vijana waliodaiwa kuvamia maeneo ya migodi.

Mganga aliyabainisha hayo jana wakati wa hafla ya ufunguzi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ya Wilaya ya Kahama iliyohudhuliwa na mahakimu na mawakili kutoka mikoa ya Shinyanga, Mara, Serengeti, Simiyu na Geita.

Alisema washtakiwa 147 wamefutiwa mashtaka yaliyokuwa yakiwakabili, 90 wakitoka Wilaya ya Kahama na 57 mkoani Shinyanga na makosa yalifutwa ni uvamizi, mauaji, wizi, ukamataji wa pombe haramu ya gongo.

Hata hivyo, DPP Mganga alisema wale walioshtakiwa kwa tuhuma za ubakaji na mapenzi dhidi ya wanafunzi hawawezi kufutiwa mashtaka.

"Mwaka jana nilifika kwenye Gereza la Kahama na kuwafutia mashtaka baadhi ya washtakiwa wakiwamo vijana wanaovamia maeneo ya migodi midogo. Cha kushangaza mwaka huu, kijana mmoja niliyemwachia mwaka jana, nimemwachia tena mwaka huu," alisema.

"Hatuwezi kuendelea kuwafutia mashtaka wahalifu kila mwaka kwa makosa ambayo yanajirudia, hivyo tuwalee watoto wetu katika misingi mizuri hasa ya kidini na kuwakumbusha kufuata sheria za nchi, ili uhalifu katika maeneo yetu yasiendelee kujitokeza.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Amon Mpanju, alisema lengo la ufunguzi wa ofisi hiyo wilayani hapa ni kusogeza huduma karibu na wananchi na kuwaondolea gharama za kusafiri kwenda ofisi ya mashtaka mkoani Shinyanga hawa wananchi kutoka halmashauri za Msalala, Ushetu na Kahama Mjini.

Aidha, alisema mpaka sasa wameshafungua ofisi za mashtaka 12 katika mikoa 25 Tanzania Bara na kuwataka wakurugenzi wa halmashauri kutenga vyumba kwenye ofisi zao kwa ajili ya ufunguzi wa ofisi za mashtaka ikiwa ni pamoja na kutenga kiwanja cha ujenzi wa ofisi baadaye.

Naibu Msajili wa Mahakama Kuu Kanda ya Shinyanga, Romuli Mbuya, alisema Wilaya ya Kahama imekuwa ikipokea mashauri 900 kwa mwaka huku Shinyanga ikipokea mashauri 1,300.

Alisema uwapo wa ofisi hiyo utasaidia kupunguza wimbi la mashauri na kutatuliwa kwa wakati.

# Tigo, Samsung zazindua Samsung Note 20, Samsung Note 20 Ultra

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Tigo kwa kushirikiana na Samsung Electronics imezindua simu janja aina ya Samsung Note 20 na Samsung Note 20 Ultra.

Ushirikiano huo ni sehemu ya mkakati wa Tigo wa kuongea matumizi ya mtandao wa 4G na kuchangia ukuaji wa teknolojia ya kidigitali nchini.

Meneja wa Bidhaa za Intaneti wa Tigo, Mkumbo Myonga, akizungumza wakati wa uzinduzi wa simu hiyo alisema: "Ni jambo kubwa sana kwetu kuchaguliwa na Samsung kuwa wa kwanza kuzihifadhi na kuuza simu za Samsung Note 20 na Samsung Note 20 Ultra kwenye soko la Tanzania. "Hii inaonyesha imani yao kwetu juu ya chaneli kubwa za usambazaji tulizonazo na pia kupitia timu yetu ya huduma kwa wateja inayotoa huduma zenye ubora wa hali ya juu."

Aliongeza kuwa: "Lengo letu ni kuchochea mageuzi ya kidigitali katika maisha ya watu nchini ndiyo maana tumeungana na Samsung ili kuongeza idadi ya umiliki wa simu janja pamoja na matumizi ya data ili kuhakikisha watu wengi zaidi wanafikiwa na teknolojia hii."

Muyonga alisema Tigo inalenga kuongeza ueneaji wa simu janja nchini huku ikihakikisha wateja wanafurahia huduma za kidigitali kupitia mtandao mkubwa wa 4G ndiyo maana inatoa GB78 za intaneti kwa mwaka mzima kwa wateja wote watakaonununa Samsung Note 20 na Samsung Note 20 Ultra.

Meneja Mkaazi wa Samsung Tanzania, Suleiman Mohamed, alisema Samsung imezindua simu ya Samsung Note 20 na Samsung Note 20 Ultra toleo jipya duniani ambayo itabadilisha namna ambavyo watu wanavyoishi na kuufurahia ulimwengu.

"Tukiwa tunaingia kwenye muongo mwingine, kuna mabadiliko makubwa kwenye sekta ya mawasiliano na namna watu wanavyo ujua na kuufurahia ulimwengu. Samsung inahakikisha inatoa teknolojia na vifaa vya kisasa zaidi ili kuendana na mabadiliko hayo.Kwa kutumia camera yenye mfumo wa AI unaweza kupata kila tukio na kuungana na uwapendao bila mipaka," alisema Mohamed.

Simu ya Samsung Note 20 itauzwa kwa Sh. 2,480,000, na Samsung Note 20 Ultra kwa Sh. 3,185,000.

# Mbaroni tuhuma kujipatia fedha kwa udanganyifu

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

JESHI la Polisi mkoani Morogoro linamshikiria Kelvin Kanola, Mkurugenzi na Mratibu wa Kampuni ya Chia Morogoro na wenzake watatu kwa tuhuma za kujipatia Sh. milioni 476 kwa njia ya udanganyifu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbroad Mutafungwa, alisema jana kuwa watuhumiwa hao walijipatia fedha hizo kutoka kwa zaidi ya wakulima 200 kutoka mikoa ya Morogoro na Dar es Salaam ambao walikuwa wakichanga kiingilio cha Sh. millioni 1.5 na kuahidiwa kuvuna mara mbili zaidi kwa muda mfupi.

Alisema kituo hicho cha mauzo na ununuzi ya mbegu za chia, kilisajiliwa Julai, 2019 kwa jina la Amosi Balele kikiwa na watu 10 akiwamo Kanole, huku akibainisha kuwa baadhi yao wakiwa watu maarufu na wenyeji wa mkoa wa Morogoro.

"Katika kipindi cha mwaka mmoja, walifanikiwa kuwashawishi wakulima 200 na kukusanya zaidi ya Sh. milioni 476 ambazo zilihifadhiwa kwenye akauti ya benki ya Equity bila kutoa gawio kwa wananchama wao kama walivyowaahidi," alisema Mutafungwa.

Alisema watuhumiwa hao walitumia pesa hizo kufanya matumizi yasiyo sahihi kwa kununua vyombo vya usafiri na satrehe bila kutoa gawio jambo liliwatia shaka wananchama na kuamua kutoa taarifa polisi.

Kamanda Mutafungwa alisema baada ya kufunguliwa shauri la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu, watuhumiwa hao walitoroka walikamatwa katika maeneo tofauti nchini.

"Tumewakamata wakiwa na vielelezo ambavyo ni gari aina ya Peugeot lenye namba za usajili T264 DPS lenye thamani ya Sh. milioni 19 na viroba 10 vya mbegu za chia. Upelelezi unaendelea na ukikamilika tutawafikisha mahakamani," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF ihakikishe kero hizi hazijitokezi tena Ligi Kuu

**PAZIA** la Ligi Kuu Bara litafunguliwa rasmi kesho kwa timu 12 kushuka dimbani katika viwanja sita nchini kabla ya raundi ya kwanza kukamilika keshokutwa kwa KMC FC kuikaribisha Mbeya City Uwanja wa Uhuru, huku Kagera Sugar ikiwa katika dimba la Kaitaba mjini Bukoka ikiialika JKT Tanzania wakati huo Azam FC ikiwa mwenyeji wa Polisi Tanzania.

Kwa kesho, mabingwa watetezi wa ligi hiyo, Simba watakuwa wageni wa Ihefu FC katika Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, wakati watani zao Yanga wakiwaalika Tanzania Prisons kwenye dimba la Mkapa jijini Dar es Salaam, huku Mtibwa Sugar ikiwa mwenyeji wa Ruvu Shooting katika Uwanja wa CCM Gairo.

Mechi zingine zitakazopigwa kesho itakuwa kati ya Namungo FC ambayo itaialika Coastal Union kwenye Uwanja wa Majaliwa mkoani Lindi, huku Biashara United ikiwa mwenyeji wa Gwambina FC katika dimba la Kumbukumbu ya Karume mjini Musoma wakati Dodoma Jiji ikishuka katika uwanja wake wa nyumbani mjini Dodoma kuikaribisha Mwadui FC.

Tofauti na msimu uliopita wa 2019/20 ambao ulishirikisha timu 20, msimu unaoanza kesho wa 2020/21, zitashuhudiwa timu 18 zikiwani taji hilo ambalo bingwa huiwakilisha nchini kwenye michuano ya kimataifa, Ligi ya Mabingwa Afrika.

Matarajio yetu msimu huu ni kushuhudia ligi bora zaidi hasa kutokana na usajili uliofanywa na timu shiriki, kupungua kwa timu, lakini maandalizi makubwa kwa kila klabu, hivyo ni vema Shirikisho la Soka nchini (TFF) likaongeza umakini katika kushughulikia changamoto zilizojitokeza msimu uliopita na kugeuka kero kubwa kwa klabu, mashabiki na wadau wa soka kwa ujumla.

Ni ukweli usiopingika kuwa, kutokana na klabu zetu kusajili nyota wa kiwango cha juu kutoka nje ya nchi, Ligi Kuu Bara itakuwa ikifuatiliwa na mashabiki ndani na nje, hivyo itakuwa ni aibu kama baadhi ya kero zilizojitokeza msimu uliopita hazitashughulikiwa mapema na kumalizwa kabisa.

Awali ya yote, tunafahamu ratiba ya Ligi Kuu imetoka kabla ya ile ya Shirikisho la Soka Afrika (Caf) pamoja na ile ya Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), hivyo tunatarajia Bodi ya Ligi nchini (TPLB) itafanya mabadiliko ya ratiba kadri ligi hiyo itakavyokuwa ikiendelea.

Pamoja na changamoto hiyo, hatutarajii kuwapo kwa viporo vingi kwa timu zitakazoshiriki michuano ya kimataifa, Simba inayoipeperusha bendera ya nchi kwenye Ligi ya Mabingwa na Namungo FC yenye dhamana hiyo kwa upande wa Kombe la Shirikisho Afrika.


Kero nyingine ambayo TFF na TPLB, ikishirikiana na Chama Cha Waamuzi Tanzania (FRAT), ni kuhakikisha waamuzi wanaopewa dhamana ya kuchezesha ligi hiyo wanafuata sheria 17 za soka duniani, ili kupatikana kwa mshindi halali na si kuonyesha mapenzi yao kwa kuzibeba baadhi ya klabu.

Tatu ni changamoto ya viwanja, ni uwazi usiopingika kuwa viwanja vingi nchini ni vibovu, ukiondoa ule wa Azam FC (Chamazi), unaotumiwa na Kagera Sugar (Kaitaba), Uhuru na ule wa Mkapa jijini Dar es Salaam, vingine vilivyosalia ni sawa na maji kupwa kujaa. vilivyosalia mara nyingi huonekana kidogo afadhali kwa muda mfupi na baada ya raundi kama nne ama tano za ligi wamiliki hushindwa kuvitunza na matokeo yake kugeuka kuwa kama machungio ya ng'ombe.

Hivyo, ni vigumu kupata bingwa halali kama baadhi ya timu zitashindwa kupata matokeo tarajiwa kutokana na ubovu wa uwanja, kulemewa na ratiba ama mwamuzi kuzifinyanga sheria 17 za soka.

Tuna uhakika kama changamoto hizo zikifanyiwa kazi, ligi yetu itazidi kuwa miongoni mwa ligi bora Afrika na kuvutia wawekezaji wengi zaidi, hivyo TFF na TPLB hawana budi kuhakikisha wanatokomeza kero hizo kabisa. Tunazitakia ligi njema klabu zote 18 zinazoshiriki.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Barnabas Maro

# Mvutano huu Simba, Yanga vipi?

**'MVUTANO'** ni hali ya kuhitilafiana kuhusu jambo; hali ya nguvu mbili kila moja kupeleka kwake. Ndivyo zilivyo Simba na Yanga. Timu hizi zaitwa 'watani wa jadi' ila sikubaliani na wanaoziita hivyo. Kwa hakika zapaswa kuitwa 'wapinzani wa jadi' na si vinginevyo.

Maana ya 'utani' ni maneno au vitendo vya dhihaka; mzaha. Tabia ya watu kufanyiana masihara kwa lengo la kuambiana ukweli na kuimarisha uhusiano wao. Pia ni taratibu au desturi za kimila ambazo zinawafanya watu wanaojuana waweze kuambiana na kutendeana jambo lolote la mzaha bila kuleteana chuki au kero.

Je, ni kweli Simba na Yanga hudhihakiana? Hufanyiana masihara kwa lengo la kuambiana ukweli na kuimarisha uhusiano wao? Mambo wanayofanyiana ndio 'taratibu na desturi za kimila' zinazowafanya watu wa pande hizo mbili 'kutendeana jambo lolote la mzaha bila kuleteana chuki au kero?' Mbona timu moja inapokuwa kwenye matatizo upande mwingine huzusha maneno ya kejeli na wakati mwingine hata matusi kwa upande mwingine! Huo ndio 'utani wa jadi?'

Tabia za baadhi ya wanachama na mashabiki wa timu hizo ni ujinga uliokithiri, chuki na kutoelewa maana ya utani. Maneno: 'Watani wa jadi' si sahihi kwani 'jadi' ni asili ya mtu. Mwenendo wa mtu; mambo ya asili ambayo watu wamerithi kutoka kwa mababu zao.

Mbona zamani wanachama na mashabiki wa timu hizo hawakufanyiana chuki kama wanavyofanyiana sasa? Nakumbuka kitendo nilichofanyiwa na shabiki wa Simba wakati timu hiyo ilipoifunga timu yangu (Yanga) mabao 6-0 kwenye Uwanja wa Mkapa pale Temeke. Shabiki huyo alifika nyumbani kwangu akiwa na chupa sita zilizojaa bia.

Hakunikuta lakini alimwambia mke wangu anaziweka chupa zile za bia kando ya mlango ili nitakaporejea mke wangu amwonyeshe. Eti ili niondoe majonzi ya kufungwa mabao sita kwa sifuri. Ingawa siku zile nilikuwa mnywaji, sikuweza kunywa kwa jinsi timu yangu (Yanga) ilivyofungwa mabao 7-0 na wapinzani wetu - Simba!

Huo ndio utani wa jadi badala ya kuchekelea mtani anapofungwa na timu inayotoka nje ya Tanzania, tena kwa kushangilia na kutukanana matusi ambayo nimejaribu kutafuta herufi zake, lakini nimeshindwa kuzipata. Upuuzi huu umewatawala sana wanachama na mashabiki wa timu za Simba na Yanga. Nionavyo hautaisha.

Msimu uliopita Simba ilitwaa vikombe na ngao zote isipokuwa Kombe la Mapinduzi lililotwaliwa na timu ya Mtibwa kwa kuifunga Simba bao 1-0. Kabla ya Simba kutwaa Ngao ya Jamii ilipoifunga Namungo kwa mabao 2-0, timu hiyo na Yanga ndizo zilizotwaa Ngao ya Jamii mara nne kila moja, lakini Simba ilipoifunga Namungo ikaweka rekodi ya kutwaa Ngao hiyo mara tano wakati Yanga ilitwaa Ngao hiyo mara nne tu.

Yanga ilikuwa ya kwanza kutwaa Ngao ya Jamii mwaka 2001, lakini ilipokonywa na Mtibwa Sugar hata hivyo mwaka 2010 ilitwaliwa na Yanga kabla ya kupokonywa na Simba kwa misimu miwili mfululizo. Yanga ikaipokonya Simba kwa kutwaa Ngao hiyo kwa miaka mitatu mfululizo - 2013, 2014 na 2015. Ilinyang'anywa na Azam mwaka 2016. Tangu mwaka 2017, 2018, 2019 na 2020 Ngao ya Jamii imekuwa mikononi mwa Simba. Kwa hiyo timu iliyotwaa Ngao ya Jamii mara nyingi zaidi ni Simba iliyotwaa mara sita ikifuatiwa na Yanga iliyotwaa mara tano. Azam na Mtibwa Sugar zimetwaa Ngao ya Jamii mara moja moja tu. Ina maana timu ngumu kuwania Ngao ya Jamii ni Simba, Yanga, Mtibwa Sugar na Azam tu ndizo zinazokabidhiana Ngao ya Jamii?

Kwa upande mwingine, Simba na Yanga zimekuwa zikinyang'anyana wachezaji tangu zamani. Emmanuel Albert kwa mfano, alikuwa mchezaji wa Yanga lakini alitwaliwa na Simba. Hata hivyo, Simba ilipocheza na Yanga akiwapo Emmanuel aliyetoka Yanga, Simba ilifungwa mabao 5-0 kwenye Uwanja wa Karume jijini Dar es Salaam. Kama hiyo haikutosha, Yanga wakamchomoa Gilbert Mahinya kutoka Simba. Hali ya kunyang'anyana wachezaji kati ya Simba na Yanga haikuanza jana wala juzi kwani imekuwa hivyo kwa miaka nenda rudi.

Sasa timu hizo zanyang'anyana wachezaji, hasa wa nje ya nchi wanapokuwa huko huko kwao, au kutoroshwa wanapotua kwenye uwanja wa ndege jijini Dar es Salaam na bandarini kwa wale wanaotoka Zanzibar. Wahenga walisema "Fedha ilivunja nguu, milima ikalala." Maana yake pesa zina uwezo wa kuivunja milima na vilima. Methali hii hutumiwa kupigia mfano uwezo wa fedha. Mtu akiwa na pesa anaweza kufanikiwa kufanya mambo ambayo asingeweza kufanya wala kudhania kufanya.

HABARI PICHANI

# ZIARA YA OFISA MTENDAJI MKUU WA BENKI YA NCBA KATIKA VYOMBO VYA HABARI VYA IPP



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NCBA, Margaret Karume, akipata maelezo kutoka kwa Meneja wa Kiwanda cha Uchapishaji cha kampuni ya The Guardian Ltd, Balasubramaniyan Venkadachalam (kushoto), alipotembelea vyombo vya habari vya IPP, Mikocheni jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkurugenzi wa IPP, Joyce Luhanga na Mkuu wa Masoko, Mawasiliano na Uraia wa benki hiyo, Caroline Mbaga.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki hiyo, Margaret Karume, akifurahia jambo alipotembelea studio za East Africa Radio.



Mkurugenzi wa Radio One, Deogratius Rweyunga, akifafanua jambo kwa Margaret Karume, alipotembelea studio za redio hiyo.



Margaret Karume, akiwa katika studio za Capital Radio.



Margaret Karume (katikati), akifurahia jambo na Mkurugenzi Mtendaji wa East Africa Televisheni na Radio, Regina Mengi (kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa ITV/Radio One na Capital TV/ Radio, Joyce Mhavile.




Margaret Karume akijaribu kusoma taarifa ya habari katika studio ya ITV. Kushoto ni Mkurugenzi wa Chaneli za ITV na Capital TV, Macharia Koigi. **PICHA ZOTE: JOHN BADI**

## Daktari asisitiza unawaji mikono

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MGANGA Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Faustine Ndugile, amewataka walimu wa shule za msingi na sekondari mkoani hapa kuendelea kuwasisitiza wanafunzi kuendelea kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni ili kuepuka magonjwa ya mlipuko.

Amesema licha ya corona kuisha nchini, unawaji mikono unapaswa kusisitiza kwa kuwa kufanya hivyo, kutasaidia kuwaepusha na magonjwa ya mlipuko, kikiwamo kipindupindu ambacho kinatokana na ulaji wa kinyesi.

Dk. Ndugile alisema hayo jana wakati akizungumza na Nipashe, namna wanavyoendelea kupambana kudhibiti magonjwa ya mlipuko mkoani hapa.

Alisema wanaendelea kusisitiza unawaji mikono shuleni ili kuwaepusha wanafunzi na ulaji wa kinyesi pale wanapotoka kujisaidia na tabia ya ulaji vyakula ovyo bila kuzingatia usafi, hasa wanapokuwa katika mazingira ya shuleni.

"Katika harakati za kuendelea kupambana na magonjwa ya mlipuko mkoani Shinyanga, bado tunaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuzingatia usafi, ikiwamo shuleni maeneo ambayo ni hatari kwa magonjwa hayo," alisema.

"Licha ya wanafunzi kula kinyesi, hata walimu nao wanaweza kukila kupitia kwa wanafunzi wakati wa kusahihisha madaftari kwani lazima alambe kidole ndipo afunue daftari hapo tayari atakuwa amekula kinyesi. Ndiyo maana tunasisitiza unawaji wa mikono uendelee licha ya corona kuisha," aliongeza.

Pia alisema tatizo linalosababisha kutokea magonjwa ya mlipuko ni uchafu na kwamba wananchi wakizingatia usafi, magonjwa hayo hayatakuwapo na watabaki kuwa salama.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Buhangija, Manispaa ya Shinyanga, Selemani Kipanya, alisema bado wanaendelea na utaratibu wa wanafunzi kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka na chooni kuna tangi la maji lita 500 kwa ajili ya kuimarisha usafi zaidi.

# Uboreshaji mazingira wawezesha ustawi NGO

**Na Mwandishi Wetu**

KUTOKANA na serikali kuboresha mazingira ya kufanya kazi, mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO) yameendelea kukua siku hadi siku kwa kusaidiana na serikali katika sekta mbalimbali.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Dk. John Jingu, alisema hayo jana wakati akifungua mafunzo kwa wasajili wasaidizi wa NGO ngazi za mikoa na halmashauri kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro na Tanga yanayoendelea jijini Dar es Salaam.

Dk. Jingu alisema serikali imekuwa ikiandaa mazingira wezeshi kwa NGO kufanya kazi kwa tija ili kutoa mchango kwa maendeleo ya nchi.

"Mazingira haya mazuri ndiyo yanaiwezesha sekta ya NGO kukua na kustawi siku hadi siku na kutoa mchango katika maeneo mbalimbali nchini ikiwamo sekta ya ajira," alisema Dk. Jingu.

Alisema katika kuboresha mazingira hayo, zimeundwa sheria, sera na kanuni mbalimbali ili kuendana na mazingira yaliyopo ikiwamo kuwezesha mashirika hayo kusimama kama taasisi zinazojisimamia.

Dk. Jingu aliwasisitiza wasajili wasaidizi kuhimiza uwazi na uwajibikaji kwa lengo la kuifanya sekta hii kuaminika kwa wananchi na mchango wake uwe na thamani kwa jamii.

"Uwazi na uwajibikaji ni msingi imara wa utawala bora na nchi yetu imejikita katika kujenga misingi ya utawala bora kwenye nyanja zote ikiwamo mashirika yasiyo ya kiserikali. Lengo letu ni kujua mchango wa mashirika haya nchini," aliongeza Dk. Jingu.

Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dk. Laurean Ndumbaro, aliwataka washiriki kusimamia sheria, taratibu, kanuni na miongozo ya uendeshaji wa NGO katika maeneo yao sambamba na miongozo na maadili ya utumishi wa umma.

"NGO zisaidie kujenga uzalendo zaidi kwa Watanzania wanaoheshimu mila na desturi zao. Muangalie shughuli wanazozifanya ziendane na malengo ya nchi yetu," alisema.

Dk. Ndumbaro aliwataka wasajili wakumbuke sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma katika majukumu yao ya usajili wa NGO.

"Kuwateua kuwa wasajili wasaidizi ni kuzingatia matakwa ya kanuni za utumishi wa umma, hivyo mambo mengi yanawaongoza katika usajili wenu hasa sheria, sera ya NGO, kanuni zinazoongoza utendaji wa NGO pamoja na miongozo inayotolewa na Wizara ya Afya chini ya Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii," alisisitiza.

Awali, Msajili wa NGO, Vickness Mayao, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wasajili wasaidizi walioteuliwa ili kutekeleza majukumu yao na kuhakikisha jamii iliyokusudiwa inapata maendeleo.

Alisema serikali katika kusimamia uratibu wa mashirika hayo imefanya maboresho mbalimbali katika sheria, kanuni na kuandaa mwongozo wa uratibu wa mashirika yasiyo ya kiserikali. Mabadiliko hayo yameenda sambamba na uteuzi wa wasajili wasaidizi katika ngazi za mikoa na halmashauri," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Dk. Richard Sambaiga, akitoa neno la shukrani, alisema wasajili wanawajibika kufahamu taasisi yoyote inayoingia kwenye maeneo yao.

"Sisi ni kama mabalozi, isije taasisi kwenye idara yoyote bila sisi kuwa na taarifa," alisema.



Mwanasheria kutoka Ofisi ya Msajili wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Faki Shaweji, akitoa mada kuhusu dhana, sheria na kanuni za mashirika hayo, kwa wasajili wasaidizi wa ngazi za mikoa na halmashauri za mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro na Tanga katika mafunzo yanayofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: WAMJW**

# TBS yataka matumizi vifaa vyenye ubora kwenye ujenzi

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

WAHANDISI, makandarasi na wadau wengine katika sekta ya ujenzi wametakiwa kutumia vifaa na bidhaa zilizothibitishwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) katika shughuli zao ili miradi wanayotekeleza ikidhi ubora unaotakiwa.

Wito huo ulitolewa jana na Mkurugenzi wa Upimaji Ujenzi wa TBS, Johaness Maganga, wakati akizungumza kwenye Maadhimisho ya Wiki ya Wahandisi yanayofanyika jijini hapa.

Mhandisi Maganga alisema ili kupata bidhaa bora zenye viwango vinavyokidhi mahitaji ya ujenzi, ni muhimu wadau wakalitumia shirika hilo kwa kuwa ndilo lenye dhamana ya kusimamia ubora bidhaa na kwamba limekuwa likifanya hivyo kwa weledi mkubwa.

"Moja ya kazi tunazozifanya ni kudhibiti ubora wa vifaa vinavyotumika kwenye sekta ya ujenzi. Iwe ni vile vinavyotengenezwa ndani au vinavyotoka nje ya nchi," alisema Mhandisi Maganga.

Alisema wako kwenye maadhimisho hayo jijini Dodoma kwa ajili ya kutangaza shughuli wanazofanya kama shirika la viwango nchini.

Maganga alisema moja ya shughuli wanazofanya ni za kudhibiti ubora wa bidhaa, zikiwamo za sekta ya ujenzi na pia wanadhibiti ubora wa vifaa ambavyo vinatumika katika miradi mbalimbali ya serikali na ya watu binafsi.

Alisema kuna bidhaa zinazotengenezwa nchini na zingine zinatoka nje, hivyo zinapimwa ili kujiridhisha kama zinakidhi viwango.

Kwa upande wa bidhaa zinazotengenezwa nchini, alisema wanatoa leseni za ubora kwa bidhaa zinazokidhi ubora na wamekuwa wakienda kwenye masoko na kufanya ukaguzi kwa vifaa au bidhaa ambazo zipo sokoni, lakini hazijapitia TBS.

Kwa vifaa vinavyotoka nje, Mhandisi Maganga, alisema wanavikagua bandarini na vingine vinapimwa na mawakala wao ambao wanafanya kazi nje ya nchi baada ya kupewa jukumu hilo na shirika. Alisema mawakala hao wamekuwa wakipima bidhaa hizo kabla ya kuingizwa nchini.

Kwa upande wa bidhaa ambazo zinaingizwa nchini kabla hazijapimwa, alisema zinapimwa hapa hapa nchini.

"Kwa hiyo Shirika la Viwango huwa tunachukua sampuli bandarini tunazipeleka kwenye maabara zetu kwa ajili ya kuzipima ili kujiridhisha ubora wake," alisema.

Kwa bidhaa zinazokuja na vyeti vya kuthibitishwa ubora wake kutoka nje ya nchi vinavyojulikana kama 'Certificate of Conformity' (CoC), alisema mara nyingi wanachukua sampuli kwa ajili ya kujiridhisha kwenye maabara za TBS kama waliopima walitoa cheti kwa bidhaa ambazo kweli zilikidhi viwango.

# Kijazi ataka ubunifu kuepuka utegemezi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIBU Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, amewataka wahandisi kwa kushirikiana na wataalamu wa fani zingine nchini, kutafiti, kubuni na kuanzisha mifumo ya kiteknolojia ili kuondokana na utegemezi wa teknolojia kutoka nje.

Balozi Kijazi alisema hayo jana jijini hapa alipokuwa akifungua mkutano wa mwaka wa Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB) wenye kaulimbiu Mapinduzi ya Nne ya Viwanda Katika Kufikia Malengo Endelevu ya Dunia.

Alisema ili kufikia mapinduzi ya uchumi wa viwanda ni vyema wahandisi hao wakasaidia nchi kufikia azma hiyo kwa kujiandaa kiteknolojia na kubadili mfumo wa elimu ya uhandisi, ili iendane na mabadiliko ya sasa.

"Nitoe angalizo huwezi kuingia kwenye teknolojia ni lazima kujiandaa. Utoaji wa elimu ya uhandisi uzingatie mabadiliko ya viwanda awamu ya nne. Wahandisi mnatakiwa kushirikiana na wataalamu wa fani nyingine, muwe watafiti na wabunifu kuanzisha mifumo yetu ya kiteknolojia bila kutegemea nchi nyingine," alisema.

Alisema si vyema kutegemea kila teknolojia zinazotoka nje ya nchi kwa kuwa zingine zina madhara.

"Na hili linawezekana, mimi nina mfano, hii mifumo ya malipo kwa miaka mingi tumekuwa tukinunua kutoka nje ya nchi, serikali tukaamua kuimarisha chombo chetu e-Government (serikali mtandao). Mifumo mingi ya serikali imetengenezwa hapa nchini na tunaondokana na huo utegemezi," alisema.

Alibainisha kuwa matumizi ya teknolojia yanaendelea kukua na sasa dunia iko kwenye hatua ambayo roboti zinatumika kuzalisha viwandani na kutoa huduma za matibabu kwa niaba ya binadamu.

Kijazi alisema serikali imeendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda na tangu imeingia madarakani serikali ya awamu ya tano, viwanda vipya vilivyojengwa ni 8,477 kati ya hivyo, viwanda vikubwa ni 201, vya kati 460, vidogo 3,406 na vidogo zaidi 4,410.

Alisema ujenzi wa viwanda hivyo umeongeza ajira za moja kwa moja za viwandani kutoka 254, 786 mwaka 2015 na kufikia 482,601 kwa mwaka 2020, hivyo kuna ongezeko la ajira takribani 227,000.

"Ajira zimeongezeka mara mbili ikilinganishwa na miaka mingine iliyopita. Hayo ni mafanikio makubwa na zitaendelea kuongezeka kadri viwanda vinapojengwa. Lakini kuna ajira zisizo za moja kwa moja nyingi zimezalishwa. Hivi viwanda vinapojengwa vitahitaji huduma za kihandisi na ni vyema kujiandaa," alisema.

Katika hatua nyingine, Balozi Kijazi aliagiza bodi hiyo kufuatilia kwa karibu na kuwachukulia hatua haraka wahandisi wanaokiuka miiko ya taaluma yao na kuisababishia serikali hasara.

Alisema kuna wahandisi wanafanya kazi kinyume na maadili na viapo vyao na kwamba bado kuna jukumu la kuhakikisha wanafuata maadili na kuyasimamia.

"Wapo wanaoenda kinyume na viapo vyao, hivyo kuharibu taswira ya uhandisi na kuitia serikali hasara. Kama umepewa mradi umetekeleza chini ya viwango, inabidi utekelezwe tena kwa fedha nyingine.

"Bodi mnalo jukumu la kuwafuatilia karibu ili wasikiuke maadili na miiko iliyowekwa kwa mujibu wa viapo vyao na wale wanaofanya hivyo washughulikieni mapema la sivyo tutajenga nchi ya ajabu, jengo au barabara baada ya mwaka mmoja au miwili limejaa nyufa kila mahali," alisema.

Naye, Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Prof. Ninatubu Lema alisema bodi kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, imetoa ufadhili kwa wahandisi 304 na pia kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetoa ufadhili wa miezi sita kwa wahandisi 5, 000.



Katibu Mkuu wa Shirika la Mfumo na Muundo wa Muungano wa Jamii Tanzania (MUJATA), Hekima Malila (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu umuhimu wa kuandika habari za amani kuelekea uchaguzi mkuu wa Oktoba 28 mwaka huu. Kushoto ni Katibu wa Ulinzi na Usalama wa shirika hilo, Sadock Ntole na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Daudi Kibiki. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Katibu Mkuu awapa somo wakurugenzi maji

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WIZARA ya Maji imewaagiza wakurugenzi wa mamlaka za maji nchini kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora ya maji.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Mhandisi Anthony Sanga, alisema hayo jana alipokuwa akifungua kikao kazi cha kutathmini utendaji kazi wao wa kila siku.

Alisema kuna baadhi ya watendaji wanafanya kazi bila ushirikiano hali ambayo inapunguza tija katika kutoa huduma hiyo kwa wananchi.

"Maeneo mengi bado kuna umimi, naomba umimi huu tuumalize. Tushirikiane katika utendaji wetu kwa ajili ya kufanya kazi yetu iwe bora zaidi katika kuwatumikia wananchi," alisema.

Pia aliwataka watendaji hao kila mmoja kuhakikisha huduma ya maji ya uhakika inapatikana katika eneo lake.

"Kila mmoja naomba ajiulize maswali matatu, je, katika eneo langu wananchi wanapata huduma bora ya maji? Kama hawapati kuna mradi gani ninaoutekeleza? Na kama hakuna mradi mpango gani upo?" Alisema.

Sambamba na hayo, Sanga aliwataka wakurugenzi kusimamia miradi ya maji inayojengwa na kuhakikisha inajengwa kwa ubora na kwa thamani ya fedha iliyotumika katika mradi husika.

Awali, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Dk. Francis Michael, aliwataka watumishi wa umma kuzingatia maadili ya utumishi wa umma na kujiepusha na mihemko ya kisiasa kipindi hiki cha uchaguzi mkuu.

Alisema kuna sheria na kanuni zinazomkataza mtumishi huyo kwenye masuala ya kisiasa ikiwamo kutumia nafasi yake kwa manufaa yao au kupendelea mtu fulani.

# DC ataka kasi ujenzi wa chuo

**Na Renatha Msungu,**

KONGWA

MKUU wa Wilaya ya Kongwa, Dk. Selemani Serera, ameiagiza kamati ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) Kongwa kuhakikisha inakamilisha ujenzi huo ifikapo Septemba 30, mwaka huu.

Dk. Serera alitoa agizo hilo jana katika ziara yake ya kukagua ujenzi wa chuo hicho.

Alisema muda huo ukifika hataki kupigwa kalenda kwa kuwa vijana wengi wanasubiria chuo hicho kikamilike ili waanze kujifunza ufundi wa aina mbalimbali.

"Nawapongeza sana kwa ujenzi wa chuo hiki, lakini nawaagiza tukamilishe ujenzi kwa haraka. Baada ya siku 20 au 30 muwe mmekamilisha ili hawa vijana wanaozunguka katika eneo hili waanze mara moja kusoma. Matarajio ni makubwa kwa vijana waliopo katika eneo hili," alisema.


Mkuu huyo alisema wilaya imepanga kuboresha mfumo wa elimu kwa kuhakikisha jamii inajua umuhimu wa elimu na ufaulu unaongezeka maradufu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, Dk. Omary Mkulo, alimhakikishia mkuu huyo wa wilaya kuwa maagizo hayo kamati imeyapokea na watakamilisha ndani ya muda huo.

Alisema majengo 13 yameshakamilika na sasa wanaendelea na ukarabati wa mwisho kuhakikisha kwamba majengo yanakuwa na ubora unaotakiwa.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi wa Chuo hicho, Paschalina Duwe, alisema Sh. bilioni 2.137 zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo na hadi sasa zimetumika zaidi ya Sh. bilioni moja kujenga madarasa 13, ambayo yako katika hatua za mwisho kukamilishwa.

"Sisi tuna tumia mfumo wa 'force account' na tulikuwa tunakabiliwa na tatizo la magari kukwama kutokana na ubovu wa barabara pamoja na ugonjwa wa corona. Lakini sasa hivi tukuhakikishie Mkuu wa Wilaya ujenzi utakamilika kwa wakati," alisema.



# Msomi atoboa siri wanawake kukosa fursa za uongozi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWANATAALUMA wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), Profesa Issa Haji Ziddy, amesema kwa miaka mingi wanawake Zanzibar wamekuwa wakipoteza fursa za uongozi kutokana na baadhi ya watu kuwa na mitazamo hasi ikiwamo kuamini mwanamke hapaswi kuwa kiongozi jambo ambalo sio sahihi.

Aliyasema hayo wakati akiwasilisha mwongozo wa utoaji elimu wa nafasi ya mwanamke na uongozi katika Uislamu kwa viongozi wa dini na baadhi ya wawakilishi kutoka asasi za kiraia katika ofisi za Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, huko Tunguu Wilaya ya Kati Unguja.

Alisema wako baadhi ya watu kwa sababu wanazozijua wao wanatumia baadhi ya aya za Quraan kuwakandamiza wanawake na kusababisha wanawake hao kupoteza fursa ambazo zingewakomboa na familia zao.

Pia alisema bado kuna baadhi ya watu wanaendelea kuamini kuwa kazi za mwanamke ni kutunza familia pekee na kunyimwa haki zake za kimsingi.

Naye Mjumbe wa Kamati ya Amani Zanzibar, Sheikh Fadhil Soraga, alisema si sahihi wanawake kunyimwa fursa zikiwamo za uongozi na wanaofanya, hivyo wanapaswa kutambua kuwa wanabeba dhima na wanapaswa kuacha mara moja.

Soraga aliwataka wanawake kupinga vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia kwa sababu baadhi yao wamekua wakijihusisha katika vitendo hivyo.

"Baadhi ya wanawake utawakuta wanacheza katika sherehe mbalimbali wakiwa wamevaa mavazi ambayo hayaendani na mila na desturi zetu," alisema.

Mchungaji Stanley Nicholas wa Kanisa la Anglikana Zanzibar, alisema ukandamizaji na udhalilishaji unatokana na watu kutokua na elimu na kukosa utayari wa kujifunza.

# Wanahabari wapongezwa kupunguza ujangili

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAANDISHI wa habari wamesaidia kupungua kwa makosa ya ujangili dhidi ya wanyamapori na kusababisha watuhumiwa wa makosa ya utakatishaji wa fedha kutiwa hatiani.

Ofisa kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Salim Hakim Msemo, alisema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari katika mafunzo ya uhifadhi wa mazingira yaliotolewa na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET) kwa kushirikiana kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID-Protect), chini ya mradi unaolenga kutoa elimu ya kutokomeza ukatili na ujangili kwa wanyamapori nchini.

Alisema licha ya kuwapo kwa sheria mbalimbali ikiwamo ya uhifadhi wa wanyamapori, pia waandishi wa habari wamefanya kazi kubwa kuripoti uhalifu wa wanyamapori na uharibifu wa mazingira, ambapo kumesaidia watuhumiwa wa rasilimali hizo kutiwa hatiani.

"Waandishi wa habari kuandika habari hasa za mazingira na uhifadhi wa wanyamapori kumesaidia kupungua kwa ujangili nchini kwa mfano, kesi ya Malkia wa Tembo ambayo iligonga sana katika vyombo vya habari," alisema.

Msemo alizitaja baadhi ya sheria zingine zilizosaidia sheria ya misitu, mazingira, uhifadhi wa taifa, sheria mahususi inayohusika na eneo la Ngorongoro na sheria ya utakatishaji wa fedha.

Naye Mwenyekiti wa chombo cha pamoja Task Force Tanzania (MNRT), Robert Mande, alisema ujangili huwiana na makosa ya kupangwa na yanahusisha watu wengi, ambao wako ndani na nje ya nchi.

"Baada ya kuona hali inakuwa mbaya vyombo vya sheria viliungana na kufanya kazi yao. Sasa matukio hayo yameondoka kwa kiasi kikubwa pia tuwapongeza waandishi wa habari kwa kazi kubwa wanayoifanya kupaza sauti zao," alisema.


Mande alisema asilimia 60 ya wanyamapori walipotea wakiwamo tembo 43,000 waliuawa katika mwaka 2010 hadi 2014.

Alisema ushirikiano kati ya vyombo vya sheria, waandishi wa habari na wadau wa mazingira umesaidia kupungua kwa ujangili na sasa idadi ya tembo imeongezeka toka mwaka 2018 hadi 2020 na kuleta matumaini makubwa nchini.

Ofisa mwandamizi kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Ally Katonya, alisema misitu ni kitu muhimu katika uhifadhi wa wanyamapori na utalii nchini.

Alisema serikali ya Tanzania ilitaifisha mali zenye thamani ya Sh. bilioni 4.7 zinazotokana na mazao ya misitu hivyo misitu ni moja ya rasilimali muhimu katika uhifadhi wa wanyamapori.

Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET), John Chikomo, aliwataka waandishi kuwaandika habari za usahihi,



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, akitia saini kitabu cha maombolezo kufuatia kifo cha Rais wa zamani wa India, Shri Pranab Mukherjee katika ubalozi mdogo wa India, eneo la Migombani, jana. Kushoto ni Balozi Mdogo wa India aliyepo Zanzibar, Shri Bhabwant Singh. **PICHA: OMPR – ZNZ**

# Masheha watakiwa kupinga udhalilishaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Dawati la Jinsia Mkoa wa Kusini Unguja, Ali Mohammed Othman, amewataka masheha wa shehia 42 za Wilaya ya Kati Unguja kufanya kazi kwa ushirikiano na waratibu kwa kupinga vitendo vya udhalilishaji.

Alisema lengo ni kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya serikali hasa katika kupiga vita vitendo hivyo.

Akizungumza katika kikao kilichowashirikisha masheha na waratibu hao, alisema ni vyema wakatambua kuwa ushirikiano katika shehia zao ni muhimu katika kutafuta mbinu na njia zitakazofichua na kuondoa vitendo hivyo mkoani humo.

Othman alisema uzoefu unaonyesha kuwa vitendo vya udhalilishaji wa wanawake na watoto huongezeka baada ya sherehe zinazofanyika, hivyo aliwataka masheha na waratibu hao kuwa tayari kupambana na vitendo hivyo hasa katika kipindi hiki cha kampeni za uchaguzi.

Alisema vijana wengi hawaendi kwa lengo la kusikiliza sera za wagombea badala yake huenda kinyume na lengo la kampeni hizo.

Pia aliwataka masheha hao kuzingatia mipaka yao na sheria wanapotoa taarifa kwa vyombo vya habari kuhusiana na watuhumiwa wa vitendo hivyo katika shehia zao. Katibu Tawala wa Wilaya ya Kati, Omar Ali, aliwataka viongozi hao kubadilika na kuwa tayari katika kutafuta mbinu zitakazowapelekea kuwabaini watu wenye viashiria vya vitendo hivyo na kusimamia kwa nguvu zao ili kuwafikisha mahakamani watakaobainika kutenda vitendo hivyo. Mwanasheria kutoka Dawati la Jinsia Mkoa wa Kusini Unguja, Sadik Ali Sultan, alisema lengo la kikao hicho ni kuwasaidia waratibu hao masuala ya kisheria kwenye matukio ya udhalilishaji ili kujua aina za makosa hayo.

Nao washiriki wa kikao hicho, walikiri kuwapo kwa vitendo hivyo kipindi cha sherehe, ambapo na kwamba walichukuwa jitihada kubwa kuhakikisha wanawakamata watendaji wa vitendo hivyo.

Nipashe BT NDANI NJE TELE





# MIAKA 20

# Utamu wa Lady Jaydee Unapowalewesha wengine

WAKATI mwanamuziki, Lady Jaydee, anatimiza miaka 20 tangu aingie katika muziki wa Bogo Fleva, msanii huyo amekuwa na mambo mengi yanayomtofautisha na wengine.

Katika mahojiano ya hivi karibuni, msanii huyo alionyesha utofauti wake na wasanii wengine baada ya kueleza mambo mazito yanayoashiria ukongwe wake, busara, uvumlivu na utulivu.

Lad Jaydee, ameeleza ndani ya miaka 20, amefanya kazi kubwa kuhakikisha nyimbo zake zinaendelea kupendwa na masahabiki wake.

Anesena siri kubwa ya nyimbo zake kuwa katika masikio ya watu, ni utundu wake wa kuziandika kutokana na matukio ya kweli yanayotokea ndani ya jamii.

"Nyimbo zangu nyingi zinatokana na matukio ya kweli o yaliyonitokea mimi au watu wengine, hii imenisaidia kupata nyimbo zenye hisia. Unapoandika ukweli mara nyingi wimbo unaishi kwa muda mrefu," anasema.

Kuhusu suala la Vanessa Mdee, kuacha muziki, Lad Jaydee, amekuwa na maoni tofauti kwani kwa upande wake yeye anamuunga mkono suala hilo, kwani safari ya muziki sio rahisi kama wanavyofikiria wengine.

"Mimi namuelewa sana Vanessa, safari sio rahisi na si kila mtu atavumilia maumivu anayopata, ni lazima tumpe moyo," ameeleza.

Aidha, msanii huyo amewataka wasanii wengine wanaopenda kufanya naye kazi ya pamoja, kutambua kuna baadhi ya vitu hawezi kuvifanya kwa sasa.

Ametaja vitu hivyo kuwa ni kucheza video zinazohusu mapenzi kwani yeye kwani umri wake hauendani na wasanii wa



# Tyler bilionea mwingine Marekani

MWIGIZAJI mkongwe kutoka Marekani, Tyler Perry, amejiunga klabu ya watu maarufu mabilionea duniani.

Kulingana na jarida la Forbes, limemtaja Perry kuwa bilionea mpya kwa kufikisha utajiri unaofikia dola Bilioni 1.4 katika makisio ya mali zake tangu mwaka 2005.

Jarida hilo linaeleza kwamba Perry afika hapo kutokana na utajiri wa mali zake ikiwamo studio yake ya utengezaji wa filamu yenye thamani ya dola milioni 320, vipindi vya TV, michezo na vitu vingine.



## Usher atarajia mtoto mwingine

MWANAMUZIKI mkali wa Marekani, Usher Raymond, anatarajia kupata mtoto na mpenzi wake Jenn Goicoechea.

Kulingana na mtandao wa PageSix wawili hao wanajiandaa kumpokea mtoto wao na wameshaanza kuandaa baadhi ya vitu kwa ajili ya malezi.

Katika picha waliyoposti hivi karibuni, zikimuonyesha Jenn mjamzito na kuvaa nguo maalum kwa wanawake wenye hali hiyo.

## Yvonne kuanza upya busara

MSANII wa filamu kutoka Nollywood, Yvonne Jegede, amesema ameanza ukurasa mpya wa maisha yake baada ya kukumbana mengi katika ndoa yake.

Katika ujumbe alioweka kwenye ukurasa wake wa Istagram, Yvonne, amesema mwaka uliopota ulikuwa mgumu kwake, lakini ameamua kwenda mbele haraka.

"Miaka michache iliyopita nilipata uzoefu mwingi, ulikuwa mgumu, kufuata sheria na kushangaza, lakini sasa nimeamua kusonga mbele haraka kujenga historia yangu nzuri na familia," amesema.





## Angela awacharukia Wanigeria

MWIGIZAJI wa Nollywood, Angela Okorie, amesema Wanigeria ambao wanaomboleza kifo cha nyota wa filamu marehemu, Chadwick Boseman, ni wanafiki.

Staa huyo kupitia video iliyoposti kupitia ukurasa wake wa Instagram,amesema anashangaa Wanigeria walikuwa wapi wakati msanii huyo wa Marekani akipambana na ugonjwa wa saratani.


"Kwa kumalizia, watu husherehekea kifo kuliko maisha. Sherehekea maisha ambayo yanastahili kusherehekewa sio wakati yamekwenda. Hasa watu ambao wamefanya mengi kuweka tabasamu usoni mwako," amesema

## Omotola apata nafuu baada ya kuugua corona

MSANII nyota wa filamu Nigeria, Omotola Jalade Ekiende, na watoto wake wamepata nafuu baada ya kuugua ugonjwa wa Covid 19.

Nyota huyo wa Nollywood, kupitia ukurasa wake wa Istagram, alimshukuru Mungu kwa kumsaidia kupata nafuu ya haraka tangu wagundulike wameambukizwa virusi vya corona.

"Namshukuru Mungu kwa kunisaidia mimi na watoto wangu kupata nafuu haraka , amefanya kazi nzuri katika familia yangu, hakika Mungu ni rafiki wa kweli kama ukimuamini," ameandika Omotola.



MAKALA

# Mashimo meusi yagongana angani

## ■Athari yake yasafiri miaka bil.1
## ■Vifaa vya anga vyayumbishwa

Na Mwandishi Wetu

HUENDA wengi wanafikiria kuwa mashimo yanapatikana ardhini au duniani pekee, lakini hivi karibuni wanasayansi wa anga za juu wanathibitisha kuwapo mashimo makubwa kwenye eneo hilo.

Wanasema mashimo hayo makubwa meusi huzunguka angani na kila kinachopita karibu hunaswa na kuvutwa ndani. Hivi karibu wasomi wa teknolojia za juu waligundua kuwa yaligongana na kusababisha mshtuko wa ajabu angani na kuathiri dunia pia.

Mawimbi yaliyotokana na mgongano huo, yalisafiri kwa muda wa miaka bilioni moja kabla ya kutua ardhini.


Wanasayansi hao, wanaoeleza nguvu ya mawimbi hayo ni sawa na nishati nane za jua zikiachiliwa kwa mpigo.

Athari ya mshikano huo ilisafiri kwa takriban miaka bilioni moja hadi kufika ardhini na kuleta madhara ya kuyumbisha vifaa vya kutambua mwanga nchini Marekani na Italia.

Nguvu za mvutano huo ulitua ardhini mwezi Mei mwaka jana.

Watafiti wanasema kwamba mgongano wa mashimo hayo mawili meusi, ulisababisha kutengeneza nguvu ya kitu kimoja chenye uzito mara 142 zaidi ya ule wa jua.

Wanasayansi kwa muda mrefu wamekuwa wakifuatilia uwepo wa mashimo meusi angani ambayo yapo madogo na makubwa.



Mchoro wa mashimo meusi mawili yakikaribiana kugongana.

Mashimo meusi yanayopatikana angani ni matokeo ya nyota kulipuka na kusababisha mzunguko wa gesi inayozunguka.

Katika ugunduzi huu mpya, unaleta tabaka jipya la mashimo meusi yalio na ukubwa wa kadri na uzito kati ya mara 100 na 1,000 zaidi ya jua.

Uchambuzi huo ni wa hivi karibuni kutoka kwa kituo cha kimataifa cha LIGO-VIRGO, ambacho kinasimamia mifumo mitatu ya kutambua mawimbi ya mvuto nchini Marekani na Ulaya.

"Inashangaza kweli," anasema Prof. Nelson Christensen kutoka Côte d'Azur Observatory huko Ufaransa.

Alisema athari za wimbi hilo zilisambaa kwa miaka bilioni saba.

"Tukio hilo lilitokea kabla ya nusu ya kuundwa kwa Ulimwengu, na sasa limewahamisha wapelelezi wetu hapa duniani," ameliambia BBC.

Ilipofanyiwa uchunguzi kutumia 'Algorithms' au mahesabu ya kompyuta, ilibaini chanzo kuwa wakati wa mwisho wa mgongano wa mashimo mawili meusi yanayozunguka.

Mashimo hayo yaliyokutana na kugongana, yalikuwa moja lina uzani mara 66 kuliko ule wa jua letu, na jingine lenye uzito mara 85 zaidi ya jua.

Umbali wa mshikamano wa mashimo hayo meusi ulidaiwa kuwa kilomita bilioni trilioni 150 kutoka duniani.

Kuhusika mgongano wa kitu chenye uzito mara 85 kuliko jua letu, kumewafanya wanasayansi kuamua kushirikiana kujua nini kinatokea mara inapotokea mshtuko wa mgongano huo.

Inafahamika kwamba mlipuko wa nyota utakuwa mkubwa, ni dhahiri ukubwa wa shimo jeusi nao utaongezeka.

Lakini fizikia inayodhaniwa kufanya kazi ndani ya nyota inaonyesha uundaji wa mashimo meusi katika tabaka fulani, kati ya uzito mara 65 au 120 zaidi ya jua haiwezekani.

Nyota kama hizo hulipuka na kuangamia na haziachi chochote nyuma.

Ikiwa sayansi inasema ukweli kuhusu hatua hii, basi maelezo sahihi kuhusu uwepo wa kitu chenye uzito mara 85 zaidi ya jua, ni kwamba ilitokana na mshikano wa mashimo mawili meusi.

Profesa Martin Hendry, kutoka Chuo Kikuu cha Glasgow, Uingereza, anaamini inaweza kuwa na athari ulimwenguni.

"Tunazungumza kuhusu muungano, njia inayowezekana kutengeneza mashimo meusi makubwa," anasema na kuongeza "Nanayejua Shimo hili jeusi lenye umbo la jua lenye uzani ulio zaidi ya mara 142 ya jua?" Anahoji Prof. Hendry.

Anaeleza matukio kama hayo yanaweza kuendelea kwa kuungana na mashimo mengine makubwa meusi.

Prof. Hendry, anasema mchakato wa kujenga mashimo meusi makubwa bado unaendelea na anadhani yapo katikati ya sayari.

Hivi karibuni wanasayansi hao, waligundua uwepo wa mashimo meusi angani yakikaribiana na kuibua wasiwasi kukutana hivi karibuni ikiwa na kasi ya kukaribiana itaongezeka.



Kituo cha utafiti cha V LIGO-VIRGO nchini Italia. **PICHA ZOTE NA MTANDAO**



# Tumaini jipya tiba saratani ya matiti

## Sumu ya nyuki yagundulika kutibu

Na Mwandishi Wetu

WAGONJWA wa saratani ya matiti, sasa wamepata tumaini jipya baada ya watafiti wa Australia, hivi karibuni kugundua kuwa sumu ya nyuki wanaotengeneza asali ina tiba ya kansa ya matiti.

Katika utafiti huo uliofanywa katika maabara, imenekana sumu ya nyuki hao inaweza kuharibu seli za saratani zilizosambaa.

Utafiti huo uliofanywa na Taasisi ya Harry Perkins, magharibi mwa Australia, na kuchapishwa katika jarida la tiba asilia, inaeleza sumu hiyo ikichanganywa na kemikali aina ya melitin ina matokeo mazuri ya kutibu maradhi hayo.

Wataalamu hao wanasema licha ya ugunduzi huo kuwa wa kufurahisha, kunahitajika vipimo zaidi ili kuhakikisha usahihi wa tiba hiyo.

Wanawake ndio waathirika wakubwa wa saratani ya matiti kuliko wanaume.


Pamoja na kuwapo kwa kemikali nyingi kwenye maabara mbalimbali ambazo zinaweza kupambana na saratani, kuna chache zinazotumiwa kama tiba ya ugonjwa huo kwa binadamu.

Awali sumu ya nyuki ilijulikana kuwa na tiba nzuri kwa aina nyengine ya saratani ikiwamo ya Melanoma.

### UTAFITI UMEGUNDUA NINI?

Kwenye utafiti huo uliohusisha vipimo vya sumu za nyuki 300, nyuki wa kutengeneza asali walionekana kuwa na uwezo mkubwa wa kupambana na saratani ya matiti.

Kulingana na mwanasayansi Ciara Duffy, (25) ambaye ndiye anaongoza utafiti huo, sumu hiyo kali iligunduliwa kuwa na uwezo wa kuua seli za saratani ndani ya saa moja, bila kudhuru seli nyingine.



Hata hivyo, ufanisi wa ufanyaji kazi wake ni baada ya sumu hiyo kuongezewa kemikali nyingine.

Utafiti huo, pia ulibaini kemikali ya Melittin pekee ina uwezo katika kuharibu na kusambaratisha mfumo wa ukuaji wa seli za saratani.

Wakati kemikali ya Melittin ipo ndani ya sumu ya nyuki wa asali, pia inaweza kuzalishwa katika maabara.

### MATUMAINI YANAKUJA

Wanasayansi kwanaeleza matokeo hayo ni matokeo mapya ambayo yanaleta faraja katika kupata tiba ya ugonjwa huo ambao kwa sasa unazidi kuongezeka duniani kote.

Profesa Peter Klinken, anasema jambo la muhimu katika utafiti huo, ni kuona Melittin imefanikiwa kuingilia ukuaji wa seli za saratani ndani ya matiti ili kuzuia kuzaana.

"Inatoa mfano mzuri ni vipi kemikali asilia zinaweza kutumika kutibu ugonjwa unaoathiri binadamu," anasema Prof. Klinken.

Lakini watafiti hao wanaonya kwamba inatakiwa kupewa muda zaidi ili kuona iwapo sumu hiyo inaweza kutumika kwa kiwango gani kama tiba ya saratani.

Watafiti wengine wa saratani wanakubaliana na matokeo hayo, wakisema ni mapema sana kuthibitisha kama tiba.

Profesa Alex Swarbrick, kutoka taasisi ya tiba ya Sidney, anasema kemikali nyingi zinaweza kuua saratani ya matiti kwa wanyama aina ya panya.

Hata hivyo, kunahitajika juhudi zifanyike kuhakikisha wanafikia kiwango ambacho kinaweza kubadili tiba ya ugonjwa huo.

### UMAKINI KWA WANAWAKE

Licha ya habari njema za utafiti huo, wanawake ambao ndio waathirika wakubwa wa aina hiyo ya saratani, wanahitaji kuelewa dalili zingine ambazo zinajificha.

Kwa mfano katika utafiti mmoja uliochunguza dalili kwa wanawake 2,300, waligundua wanawake wasiokuwa na dalili za uvimbe walikuwa na uwezekano mkubwa wa kutokutana na madaktari. Wanaonya uvimbe wowote unaonekana chini ya matiti, ni lazima kwenda haraka hospitali kwa ajili ya uchunguzi.

Dalili zingine ambazo si nzuri ni mabadiliko ya muonekano wa chuchu, kuvuja damu au kutokwa na maji maji ya aina yoyote kwenye titi.

DK. Karen Kennedy, Mkurugenzi wa Taasisi ya kitaifa ya Utafiti wa Saratani nchini Uingereza, anasema "Utafiti huu unaonyesha mara kwa mara wanawake huchelewa kwenda kumuona daktari katika dalili za mwanzo."

BBC

## HABARI KIMATAIFA

# Profesa Marekani akiri kuongopa yeye mweusi

**WASHINGTON, Marekani**

PROFESA mmoja nchini Marekani, ambaye anashughulika na kazi ya kuwasaidia Waafrika wanaoishi ughaibuni, amekiri kudanganya kuwa yeye ni mweusi.

Jessica Krug, anayefundisha Chuo Kikuu cha George Washington, alisema yeye ni mzungu mwenye asili ya Kiyahudi kutoka mji wa Kansas.

"Nilijijengea maisha ya uongo kuwa mimi ni mtu mweusi, nilidanganya katika kila katika maisha yangu," aliandika profesa huyo katika ujumbe wake.

Tukio la kudanganya asili, lilitokea pia kwa mwanaharakati Rachel Dolezal, ambaye pamoja kuwa mzungu, lakini alidai yeye ni mweusi.

Mwanaharakati huyo wa haki za binadamu na mhadhiri wa masomo ya Afrika, alidanganya kwamba ni Mmarekani mwenye asili ya Afrika kwa miaka mingi.

Kulingana na makala iliyochapishwa siku ya Alhamisi, Jessica Krug alisema aliamini visivyo kuhusu utambulisho waje. "Sikuwa na haki ya kudai mimi ni Mwafrika wa kwanza kutoka Afrika Kaskazini, ni mtu mweusi mwenye asili ya Marekani, kisha mwenye asili ya Carribean kutoka Bronx", aliandika.

Alisema tabia hiyo sawa na kuleta vurugu, wizi na ulaghai mbalimbali unaotumiwa na wazungu kuendelea kunyanyasa utambulisho wa mtu mweusi na utamaduni.

Alijilaumu kutokana na udanganyifu wake huo na kuelezea ulitokana na matatizo ya akili na mfadhaiko aliopitia miaka ya nyuma.

Makala ya Krug haikutoa sababu ya uamuzi wake wa kukiri uongo, na pia kwanini sasa ameamua kusema ukweli.

Hata hivyo, mwandishi Hari Ziyad alisema uamuzi huo umewadia kwasababu amejulikana."Jess Krug ni mtu nimemuita rafiki hadi asubuhi hii aliponipigia simu na kukubali kila kitu kilichoandikwa kwenye makala. Hakuchukua hatua hiyo ili kuonekana mzuri," aliandika kwenye mtandao wa Twitter.

Kulingana na taarifa za vyombo vya habari, Krug pia alitumia jina Jessica La Bombalera katka kujitambulisha kama mwanaharakati.

**BBC.**



Timu ya waokoaji kutoka Chile, wakifanya kazi ya kutafuta watu waliokwama katika kifusi kwa kutumia skana na mbwa wa kunusa katika eneo la Mar Mikhael nchini Beirut, jana. **(PICHA: EPA)**

# Mpinzani wa Putin alipewa sumu kali

**BERLIN, Ujerumani**

KANSELA wa Ujerumani, Angela Merkel, amedai kuna ushahidi wa wazi kuwa mwanasiasa wa upinzani nchini Urusi, Alexei Navalny, alipewa sumu aina ya Novichok inayoathiri mishipa ya fahamu.

Kansela Merkel, alisema hilo lilikuwa jaribio la kuuawa kwa mwanasiasa huyo, hivyo dunia itatafuta majibu dhidi ya Urusi.

Navalny alisafirishwa hadi Ujerumani baada ya kuugua akiwa ndani ya ndege huko Siberia, mwezi uliopita na sasa bado anaendelea kupatiwa matibabu huku akiwa katika hali ya kupoteza fahamu.

Msemaji wa Urusi aliitaka Ujerumani kuishirikisha katika taarifa zake zote, huku msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje, Maria Zakharova, akilaumu madai hayo ya Novichok, hayana ushahidi wowote.

"Ukweli uko wapi, ni mchakato gani uliotumika, yaani hata mutoe taarifa?" alisema. Sumu aliyopewa Novichok,ilitumiwa pia kwa aliyekuwa jasusi wa Urusi, Sergei Skripal, na binti yake wakiwa Uingereza mwaka 2018.

**BBC.**

# Ugiriki, Uturuki watunishiana misuli

**ATHENS, Ugiriki**

WAZIRI Mkuu wa Ugiriki,Kyriakos Mitsotakis, ameonya Uturuki kuacha kuitishia nchi yake, iwapo wanataka mazungumzo ya kupunguza mivutano kati ya nchi hizo.

Kabla ya kauli hiyo, Katibu Mkuu wa muungano wa kujihami wa NATO, Jens Stoltenberg, juzi alisema Uturuki na Ugiriki ambao ni wanachama wa muungano huo, wamekubaliana kufanya mazungumzo.

Alisema anawasiliana na kila upande mara kwa mara ili kuhakikisha suluhisho linapatikana.

Nchi hizo zipo katika mvutano baada ya kugombea eneo la mashariki mwa Mediterenia ambalo lina hifadhi kubwa ya gesi. Uturuki tayari imeanza shughuli ya uchimbaji wakati Cyprus au Ugiriki wanadai wao ndio wanamiliki.

Kuna wasiwasi mkubwa kuibuka kwa vita kati ya nchi hizo mbili kama mgogoro huo hautapatapatiwa ufumbuzi.

**DW**

# Joe Biden ataka mfumo wa ubaguzi kumalizwa

**WASHINGTON, Marekani**

MGOMBEA wa urais kupitia Chama cha Democratic, Joe Biden, amesema tukio la kupigwa risasi kwa Mmarekani mweusi, Jacob Blake, kunaweza kuisaidia Marekani kupambana na ubaguzi.

Biden alisema hayo juzi katika mji uliokumbwa na vurugu wa Kenosha. Ujumbe huo unatofautiana na mtazamo wa Rais Donald Trump, ambaye aliwafananisha na waandamanaji kama magaidi wa ndani.

Katika ujumbe huo, Biden alisema ghasia zilizotokana na kitendo cha polisi kumpiga risasi Blake katika mjini huo, kinaweza kuisaidia Marekani kutafakari mfumo wake wa ubaguzi wa rangi uliodumu kwa karne kadhaa.

"Maneno ya rais ni muhimu, haijalishi kama ni mazuri, mabaya au tofauti, ni muhimu. Haijalishi kama rais anaijua au haijui kazi yake, maneno yake yanaweza kuiingiza nchi katika vita. Maneno hayo yanaweza kuleta amani pia. Yanaweza kufanya masoko yakainuka na kuanguka na yanaweza kuleta tofauti kwa jinsi tu wanavyoyasema." Alisema Biden, akiwa na familia ya Blake.

Rais Trump hakukutana na familia hiyo katika ziara yake ya majuzi.

**DW.**

## MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### VIWANJA/MASHAMBA

**KIWANJA KINAUZWA, K**IWANJA CHA COMMERCIAL 1300SQM KINAUZWA KIPO REGENT ESTATE HAKUNA DALALI TUPIGIE: 0693 689996/ 0757 129546

**NYUMBA INAUZWA,** Nyumba ya gorofa moja inauzwa, ina frem 3 za biashara zote zinawapangaji. Ipo ukonga Dar es salaam. Simu 0757 07 90 57.

### MATANGAZO MCHANGANYIKO

**FAITH BACKBORN CLINIC!!** TUNATIBU UTI WA MGONGO DISC PROBLEM KIUNO SELLULITIES GANZI PARALIZE BODY MEDICATED FULLBODY MASSAGE AND HOME SERVICES AVAILABLE 0714 919199

### NAFASI ZA KAZI

**TUNAHITAJI DEREVA WENYE SIFA ZIFUATAZO**

- UZOEFU USIOPUNGUA MIAKA 2
- UWEZO WA KUTUMIA EFD MASHINE
- UWEZO WA KUUZA MAJI YA CHUPA **SIMU: 0767 269677**


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA


### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ALOZ HOLDINGS LTD** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA DYNA YENYE NAMBA ZA USAJILI **T947 BJL.** KWA YOYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.

**TAARIFA YA POLISI: 99108513350**

115886502

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**WUZHOU INVESTIMENT COMPANY LIMITED** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **M C 504 BEP** KWA YEYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI

TAARIFA YA POLISI **KAH/RB/1297/2020**

115886902

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**TANZANIA CHINA TRADE AND TOURISM DEVELOPMENT** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI AINA YA SINORAY SR'150 -18T YENYE NAMBA ZA USAJILI **M C 862 CGH**

KWA YEYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI

TAARIFA YA POLISI **KA H/RB/1286/2020**

115887002

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MARIAM HASSAN MGALULA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA RAUM YENYE NAMBA ZA USAJILI **T463 DFT.** KWA YOYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.

TAARIFA YA POLISI: **DAR/CEN/RB/638429/2020.**

115886002

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI MIRATHI FORM II**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI TANGA**

**Usimamizi wa mirathi 14/2020**

**Ombi la HABIBA OMARI GODIGODI kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu OMARI YUSUFU GODIGODI**

**Kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA**
........................................

Watu wote wanaodaiwa kuwa uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 28/9/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 3/9/2020

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
TANGA MJINI

115887102

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**

**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**MIRATHI NA. 62 YA MWAKA 2020**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU RICHARD MGANGA NDASSA**

**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**BOB RICHARD NDASSA & WENZAKE**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa waombaji/mwombaji hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 30 mwezi wa September, 2020.
Imewasilishwa Dar es salaam, leo tarehe 3 mwezi wa Septemba, 2020.

NAIBU MSAJILI

115887202

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**

**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**MIRATHI NA. 63 YA MWAKA 2020**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**REYNALDA JOHN KAISI**

**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**MIKE M.S MWOMBEKI & MWENZAKE**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa waombaji/mwombaji hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 06 mwezi wa Oktoba, 2020.
Imewasilishwa Dar es salaam, leo tarehe 3 mwezi wa Septemba, 2020.

NAIBU MSAJILI

115887302


Uza,

Chenye Thamani Kubwa Kwa

Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa

Tupigie 0782253676



Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

# Mauaji Harusini-28

ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote. Afanye chochote kile ili awe navyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.

Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele.

Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo. Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

**Na Adam Fungamwango,**

**(0716 350534)**

Ni Fikiri huyo huyo ambaye aliangusha kifuko kwa bahati mbaya kwenye hoteli ya ABC na alipokiangalia kilikuwa ni cha sumu.

Akapatwa na wasiwasi na chakula kilicholekwa na mhudumu huyo kwa Shani. Akakipeleka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali. Vipimo vilionyesha kuwa mabaki ya chakula yalikuwa na sumu ile ile ambayo alikuwa ameiokota, ilipoanguka kwenye mfuko wa Fikiri.

Wakati Eddy akiwa anatafakari sababu ya yote yale na hatimaye kuazimia kumsaka Fikiri, leo inakuja kuonekana kuwa ameuawa.

Aliwaza kuwa vyovyote itakavyokuwa, Fikiri atakuwa ameuawa na watu waliomtuma kumuwekea Shani sumu.

Hapo ndipo alipogundua kuwa wasiwasi wake ulikuwa sahihi. Na hata maneno ya Shani kuwa ana matatizo makubwa ni sahihi pia. Eddy alijua kuwa nyuma ya pazia kuna mpango kabambe unaosukwa kuhakikisha kuwa binti yule ambaye kwa sasa ni mpenzi wake anapoteza maisha "Sababu ni nini?" Alijiuliza bila kupata jibu.

Kingine alichogundua kuwa huenda anachofahamu Shani ni kidogo tu cha mpango mzima unaosukwa juu yake.

Akagundua kuwa kumbe yupo mikononi mwa mrembo Shani kwa sababu maalum.

"Nakupenda sana Shani. Nitakusaidia." Alijikuta akiongeza kwa sauti peke yake.

****************************

Ikiwa ni mara ya kwanza Shani kwenda nyumbani kwa Eddy. Alifika akiwa na gari lake aina ya Land Cruiser. Mwenyeji wake alisimama getini kumkaribisha.

"Karibu Sherry."

"Ahsante love"

Walikumbatiana na baadaye kushikana mkono hadi sebuleni.

Kwa jinsi ilivyoonekana, pamoja na Eddy kujitahidi sana kwenye masuala ya usafi na kuweka nyumba sawa, lakini Shani aligundua kuwa nyumba ile anaishi mwanaume tu.

Na huenda labda mwanamke huwa anakwenda baada ya mwezi mmoja, au hakuna kabisa anayefika pale.

"Tunakaa sebuleni au chumbani?" Eddy aliuliza swali, lililoonekana kama la mtego.

Shani alicheka kicheko cha kimbea. "Hebu kwanza tukae hapa, yakitushinda, tutahamia sehemu ya pili."

Walikaa kwa muda wakiangalia. Ilionekana kama kila mmoja anasoma mawazo ya mwenzake.




Shani alikuwa anavutia. Alisuka nywele kwa namna inavyompendeza mwanaume yoyote. Siku hiyo alivaa fulana nyepesi ya mikono mirefu, suruali aina ya jeans, chini akivaa raba za michezo.

Alionekana kama mwanamichezo fulani hivi, lakini urembo wake haukuweza kabisa kufichika.

"Niambie mpenzi wangu." Eddy alimchokoza.

"Ninalo basi, nimefurahi leo nimekuja kwako."

"Na hutoki humu, nadhani itakuwa baada ya siku tatu, ndiyo nitakuruhusu."

Shani aliangua kicheko kikali "Wewe Eddy una vituko, ulichelewa kutembea nini?"

"Mhh, nadhani hilo swali ungemuuliza mama yangu mzazi, kuniuliza mimi ni kunionea tu."

Ni jibu ambalo lilimfanya Shani aendelee kukauka kwa kicheko.

Dakika mbili baadaye, wapenzi hao walianza kuegemeana.

"Shani, kuna siku uliniambia kitu. Na ulisema tukiwa wawili tu. Nadhani leo ingekuwa ile siku ambayo ulitaka kuniambia kitu hicho." Eddy aliuliza kwa sauti ambayo sasa haikuwa na mzaha tena.

Shani aliona kabisa kuwa mzaha umeondoka kwa Eddy, si kwa sauti tu, bali hata sura yake.

Shani alijiweka vizuri. "Ni hadithi ndefu sana Eddy."

"Najua ni ndefu, wewe niambie tu."

"Sijui nianzie wapi."

"Anzia hapo hapo."

Shani alitaka kucheka akasita.

"Eddy, kama unavvyojua sakata lote la baba yangu Patiyo kuuawa na mkewe Grace ambaye baadaye ikaja kujulikana kuwa kumbe wewe ni shangazi yangu si ndiyo?"

"Sawa."

"Na nilikwambia kuwa mama yangu alifariki wakati mimi nina miaka mitano tu."

"Ndiyo uliniambia."

"Mimi nimeumia sana kifo cha baba yangu, wala sikupenda, lakini naona kama inaniletea matatizo hivi."

"Matatizo gani?"

"Naona kama ndugu za baba wananitenga."

"Ina maana hawawasiliani na wewe, au wanakutenga vipi?"

"Unajua tangu kifo cha baba, tumezika, mpaka arobaini, naona kama wamebadilika, hawana tena ushirikiano na mimi. Hata mimi nikiwatafuta, au kutaka ushauri, naona kama vile hawako kama vile ilivyokuwa zamani. Kusema kweli hili linaniumiza sana, sijui nimewakosea nini."

Shani alisema na kuanza kutokwa machozi, akajiegemeza kwenye kifua cha Eddy.

"Usilie mpenzi. Ni mambo ya kawaida kwenye familia nyingi, hasa za Kiafrika." Alibembeleza Eddy

"Kwani unadhani hasa tatizo ni nini hadi wamebadilika?"

"Sijui, lakini kuna ndugu yao upande wa kikeni kwao, alinifuata na kuniambia kuwa dada nakwambia kitu kimoja, baba zako hawa siyo watu wazuri kwako, kuwa makini sana nao, wanaweza kuwa wanakuchekea mdomoni, lakini mioyoni kwao wana fundo kubwa. Sikumtilia maanani, lakini naona kadri siku zinavyozidi kwenda mbele ni kama nimetengwa hivi." Shani aliongea kwa sauti ya kudeka.

Mtoto wa kike yupo kwenye kifua cha mwanaume. Mwanaume aliyetokea kumpenda na kumuamini pia.

"Ndiyo maana nilikwambia kuwa mimi nimekuwa mpweke sana, mama sina, baba sina, baba zangu wadogo na ndugu hawana ushirikiano na mimi. Baba ameniachia mali nyingi, lakini bila upendo ni kazi bure. Ndiyo maana mimi nimekuona wewe unaweza kuwa msaada mkubwa kwangu, kwa ajili ya faraja na amani ya moyo."

Eddy alitoa leso na kumfuta machozi na kumbusu. "Mtoto mzuri kama wewe hupaswi kulia. Na wala huwezi kuachwa peke yako. Lakini, haiwezekani ikawa kuwa ndugu wa baba yako, wameanza kukuchukia kwa sababu mali zote utazimiliki yeye badala na wao wapate kitu?"

"Kisheria ni mimi napaswa kurithi mali zote, lakini mimi sitaki kuchukua zote, kuna sehemu nitawapa kwa sababu yule ni ndugu yao?"

"Wao wanalijua hilo?"

"Niliwaambia, sasa sijui kama ni kweli kwa sababu wananisusa kwa sababu ya mali, au kuna kitu kingine, ila sidhani."

Sasa ziara ya mikono ya Eddy ilianza kutembea kwenye mwili wa msichana huyo. Ilimfanya ashindwe kuzungumza.

"Shani, kwenye dunia hii chochote kinaweza kutokea. Na usimuamini mtu yoyote yule. Kama ndugu zako au baba zako wakubwa umegundua kuwa kama vile wameanza kukutenga, usilazimishe, kwa sasa kubali kutengwa na uwe makini nao."

"Kweli eee." Ilikuwa ni sauti ya Shani ambayo ilitokwa kwa mbali na ya kugugumia, kutokana na mpapaso wa Eddy mwilini mwake.

Mazungumzo yaliisha. Walihamia chumbani. Kila mmoja alikuwa na kiu na mwenzake.

********************************

Maelezo ya Shani alianza kumpa wasiwasi Eddy. Kama mwenyewe ameshaanza kugundua kuwa ndugu zake wanamtenga, au hawamchangamkii tena kama zamani, je ndani ya mioyo ya baba zake wadogo ikoje?

Alianza kuunganisha matukio. Hivi ni kweli baba zake wadogo wanaweza kukubali msichana mdogo kama yule kurithi mali zote? Lakini si walishaambiwa zingine watapewa? Inawezekana hawakuridhika.

Ni nini hawa ndugu wanachofikiria kwa msichana huyu? Je tukio la chakula kile cha sumu alichotaka kuwekewa siku ile na marehemu Fikiri lina uhusiano ya jambo hili?

Iwe ni baba zake wadogo, au watu wengine, lakini ni ukweli usiopingika kuwa Shani alikuwa anawindwa ili auawe. Hilo Eddy alilitambua vema.

Na ndiyo maana baada ya jana yake kulala naye mpaka asubuhi, alimshauri aliache gari lake pale nyumbani kwake na Eddy kumtaka kupanda gari lake aina ya Toyota Brevis, akimpeleka ofisini.

Ndani ya gari, kuna vitu kadhaa ambavyo Eddy alimshauri Shani aachane navyo na pia kurekebisha mwenendo wa vitu ambavyo amekuwa akivifanya au kwenda kula siku, ili kuepuka maadui ambayo wanaweza kuwa wanamfuatilia. Alikubali kufuata, ingawa yeye hakudhani kama yuko kwenye hatari kubwa kiasi hicho. Ni Eddy pekee aliyejua kuwa Shani alikuwa hatarini, lakini hakutaka kumwambia ili kutomtisha.

Kwa jinsi alivyokuwa akimweleza, Shani alimshangaa Eddy kwa kuona ana uwezo na upeo mkubwa wa mambo ua kiitelejensia kama vile askari mpelelezi.

Hata hivyo Eddy alivyokuwa akimwambia ni yale mambo ya msingi tu na si ya ndani.

Vyote hivyo vilimfanya Shani azidi kumpenda Eddy na kujiona mwenye bahati kubwa kupata mtu wa aina ile.

"Huyu ndiye mlinzi wangu, huyu ndiye mtu niliyekuwa namhitaji kwenye maisha yangu. Huyu ndiye mpenzi niliyemtaka. Na huyu ndiye nataka awe mume wangu." Alijiambia mwenyewe akiwa ofisini baadaye kuteremshwa na gari, huku na yeye akielekea ofisini. Shani pia hakujua kuwa Eddy alikuwa anafanya kazi wapi. Alichotambua kwa kuambiwa na mwenyewe kuwa ni mchakarikaji tu wa mjini maarufu kama 'mesheni tauni'.

*Itaendelea Jumamosi*



# GIROUD

## HANA HOFU NA UJIO WA WERNER

**LONDON, England**

OLIVIER Giroud amesema hana hofu yoyote ya nafasi yake pale Chelsea licha ya ujio wa Timo Werner.

The Blues walimnunua mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani, Werner baada ya kung'ara katika msimu wa 2019-20 ambao alifunga mabao 34 kwenye mashindano yote akiwa na RB Leipzig, na kuwa mfungaji wa wakati wote wa klabu hiyo ya Bundesliga.

Hata hivyo, Giroud haoni hilo kama ni tishio kwake katika nafasi ya ushambuliaji wa kati baada ya kuonyesha kiwango cha kuvutia katika kipindi cha pili cha nusu ya msimu, huku Werner mara kwa mara akipenda zaidi kucheza winga ya kushoto akiwa na klabu yake pamoja na timu ya taifa.

Giroud alifunga mabao saba katika mechi 12 wakati msimu uliporudi tena baada ya kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, na nyota huyo wa zamani wa Arsenal mwenye umri wa miaka 33, anaona kwamba bado ana nafasi kikosini hapo.

"Katika kila klabu kubwa, kuna ushindani, na hilo huwa linanipa mimi hamasa ya kupigania nafasi yangu," alisema akiwaambia waandishi wa habari wakati akiwa na timu ya Taifa ya Ufaransa.

"Sasa, mimi nina uzoefu wa kutosha na najua klabu imemleta Werner kumuweka uwanjani. Kitu kimoja kwa uhakika, tunacheza nafasi tofauti, anapenda kucheza pembeni kama alivyokuwa anafanya kwenye klabu yake na timu ya taifa.

"Kama angekuwa straika tunayefanana, ningekuwa nahofia sana nafasi yangu, lakini nafikiri kwa utofauti wa mechi na timu, tutacheza pamoja, kocha atatafuta mbinu tofauti ya kutuchezesha na nina matumaini nitacheza, kutokana na kile nilichokifanya mwaka uliopita."

Muda wa Giroud kucheza pale Chelsea ulionekana utafikia mwisho mwaka huu 2020 na awali aliwahi kubainisha kwamba alifanya "kila kitu" kujaribu kutaka kuondoka klabuni hapo.

Alianza katika mechi mbili tu za Ligi Kuu ya England kabla ya Februari, huku kocha, Frank Lampard akipenda kumtumia zaidi Tammy Abraham, lakini Chelsea iliamua kumbakiza Giroud.

Nyota huyo wa zamani wa Montpellier, alibainisha kwamba uhusiano wake na Lampard umeimarika na umempa nafasi zaidi.

"Uhusiano wangu na kocha umebadilika," aliongeza Giroud.

## THIAGO: BAYERN NI NYUMBANI KWANGU

**MUNICH, Ujerumani**

THIAGO Alcantara amedokeza kwamba, hajaondoa uwezekano wa kubaki katika klabu ya Bayern Munich.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania alikuwa na wakati mzuri chini ya kocha, Hansi Flick wakati Bayern iliposhinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na kumaliza msimu wa 2019-20 wakiwa na mataji matatu.

Thiago mwenye umri wa miaka 29, mkataba wake unamalizika Juni mwakani na amekuwa akihusishwa zaidi na uwezekano wa kwenda kujiunga na Liverpool.

Alipoulizwa kama "hakuna nafasi" ya yeye kubaki Bayern kwa msimu ujao, alijibu: "Bayern ni nyumbani kwangu na nina furaha kuwa hapa.

"Ninachofikiria kwa sasa ni kuhusu mchezo wa (Hispania) dhidi ya Ukraine. Baada ya hapo tutaona nini kitafuata."

Tangu alipowasili kutoka Barcelona mwaka 2013, Thiago amecheza mechi 235 kwa Bayern, akifunga mabao 31.

Wikendi iliyopita, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bayern, Karl Heinz-Rummenigge alisema Thiago: "Inaonyesha kama ataondoka. Natarajia kupata ofa kwa ajili ya kumsajili ndani ya siku chache zijazo."






## UNITED SASA YAAMUA KUACHANA NA GREALISH

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United imesimamisha mazungumzo ya kutaka kumsajili kiungo wa Aston Villa, Jack Grealish.

Kocha wa 'Mashetani Wekundu' hao, Ole Gunnar Solskjaer sasa ameonyesha kuridhika zaidi na usajili wa Donny van de Beek kutoka Ajax na hivyo hana mpango tena na Grealish.

Awali ilielezwa kuwa United walikuwa wanataka saini ya nahodha huyo wa Aston Villa, lakini sasa Solskjaer amesema hana nia hiyo tena.

United ilikuwa tayari kuweka mezani kitita cha pauni milioni 80 kupata saini ya kiungo huyo ambaye ameitwa kwa mara ya kwanza kwenye timu ya Taifa ya England.

Kiungo huyo alionyesha kiwango kikubwa msimu uliopita na alikiongoza kikosi chake kujinusuru kushuka daraja.

Pia mabosi wa United walikuwa wanahitaji saini ya Jadon Sancho wa Borussia Dortmund na huko dili lilikuwa gumu kwa sababu ya dau walilotajiwa kuwa kubwa.

## HABARI MICHEZO



# MANE SASA ATAJWA BARCA

**LIVERPOOL, England**

NYOTA wa Liverpool, Sadio Mane anatajwa kuingia anga za Klabu ya Barcelona ili kuziba pengo la mshambuliaji wao namba moja, Lionel Messi ambaye inaelezwa anataka kuondoka ndani ya kikosi hicho.

Mane raia wa Senegal amekuwa chachu kubwa ya mafanikio ndani ya Liverpool ambayo msimu wa 2019/20 ilitwaa taji la Ligi Kuu England baada ya kupita miaka 30 pia alikuwa kwenye kikosi kilichotwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Amekuwa akifanya kazi kwa ukaribu na nyota wa Liverpool raia wa Misri, Mohamed Salah pamoja na nyota mwingine Roberto Firmino wakiunda utatu wao matata ndani ya kikosi hicho kinachotumia Uwanja wa Anfield kwa mechi za nyumbani.

Ripoti zinaeleza kuwa Mane anataka kwenda Barcelona ili akafanye kazi na kocha mpya wa klabu hiyo, Ronald Koeman ambaye kwa sasa yupo ndani ya kikosi hicho kwa kuwa walifanya naye kazi alipokuwa akikinoa kikosi cha Southampton.

Wakati Mane anafanya kazi na kocha huyo, alifunga mabao 25 kwenye jumla ya mechi 75 alizocheza, hivyo anaamini endapo akitua hapo atapata nafasi ya kurejesha makali yake zaidi.



# SPURS YAMUWEKA SOKONI NDOMBELE

**LONDON, England**

TOTTENHAM Hotspur wapo tayari kusikiliza ofa kutoka timu ambayo inamhitaji nyota wake, Tanguy Ndombele ambaye ni raia wa Ufaransa.


Kiungo huyo alikuwa mchezaji muhimu wakati wa kocha, Mauricio Pochettino, lakini ameshindwa kupata nafasi baada ya kocha huyo kufukuzwa na nafasi yake kuchukuliwa na Jose Mourinho.

Ripoti zinaeleza kuwa kwa sasa Mourinho yupo tayari kumuuza kiungo huyo mwenye miaka 23, ikiwa tu mnunuaji atapatikana na kufikia bei ya kumnunua nyota huyo.

Kocha huyo anaamini kwamba bado Ndombele hajaweza kwenda sawa na kasi ya Ligi Kuu England hivyo ana mashaka naye.

Pia sababu nyingine iliyofanya nyota huyo awekwe sokoni kwa dau la pauni milioni 54, ni kuongeza mkwanja ndani ya timu hiyo ambayo imeyumba kutokana na janga la virusi vya corona kuvuruga mambo kwenye masuala ya mapato.

Kwa sasa nyota huyo yupo kwenye uangalizi maalumu baada ya kukutwa na virusi vya corona na hayupo katika mpango wa Mourinho ndani ya kikosi cha Spurs.



# UNITED YAJITOSA KWA UPAMECANO

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United ipo kwenye mpango wa kuinasa saini ya beki wa Klabu ya RB Leipzig, Dayot Upamecano kwa ajili ya kuongeza nguvu msimu ujao wa 2020/21.

Kocha Mkuu wa United, Ole Gunnar Solskjaer yupo kwenye mpango wa kuboresha safu yake ya ulinzi ambayo imekuwa na tatizo la umakini kwa msimu wa 2019/20.

Lengo la kocha wa United ni kumwongezea nguvu nahodha wa kikosi hicho, Harry Maguire ambaye ndiye tegemeo kwa upande wa ulinzi ndani ya kikosi hicho.

Kwa mujibu wa ESPN, Solskjaer anaamini kwamba atakamilisha dili hilo mapema kabla ya Oktoba 5, mwaka huu.

Tayari nyota huyo mwenye miaka 21, anayeshiriki Ligi ya Bundesliga, amesaini mkataba mpya na timu yake ambayo ilitinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kabla ya kutolewa na PSG ya Ujerumani, hivyo italazimika kutoa pauni milioni 53 kwa ajili ya ada ya kumpata nyota huyo.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA AHESABU SIKU AUBAMEYANG KUSAINI

●●●Nimekuwa nikipambana kuhakikisha namshawishi ili abaki, hii ni timu yake, naamini...

**LONDON, England**

MIKEL Arteta, amesema kuwa mshambuliaji wake namba moja, Pierre Emerick Aubameyang atasaini mkataba mpya hapo Arsenal ndani ya siku chache zijazo.

Arteta amekiongoza kikosi chake kutwaa mataji mawili kwa kuzifunga timu kubwa, ambapo kwenye fainali ya FA waliichapa Chelsea mabao 2-1 na kubeba kombe hilo.

Pia wakaifunga Liverpool kwa changamoto ya mikwaju ya penalti 5-4 kwenye mchezo wa Ngao ya Jamii wikendi iliyopita.

Mtupiaji wa mabao yote matatu alikuwa ni nahodha Aubameyang ambaye amekuwa akitajwa kutaka kuondoka ndani ya kikosi hicho.

Arteta alisema: "Nimekuwa nikisema jambo lilelile kuhusu Aubameyang. Ni mchezaji mzuri ambaye anaweza kucheza michezo mikubwa.

"Nimekuwa nikipambana kuhakikisha namshawishi ili aweze kubaki kwenye timu hii, naamini atakubali kusaini kwa kuwa hii ni timu yake bora na tukiwa pamoja tutafanya makubwa msimu ujao." Msimu mpya wa Ligi Kuu England unatarajiwa kuanza Septemba 12, mwaka huu, huku Arsenal ikianza na Fulham.

## KWA UFUPI

**ARSENAL, CEBALLOS KUENDELEA**
KLABU ya Arsenal inakaribia kukamilisha makubaliano ya kumsajili kwa mkopo kiungo wa kati wa Real Madrid na Hispania, Dani Ceballos kwa msimu wa pili. ***(Mail)***

**MESSI KUTOONDOKA BARCA**
BABA yake Lionel Messi amejadiliana na Barcelona kwa siku ya pili mfululizo juu ya uwezekano wa kijana wake kuihama klabu hiyo, na mlinzi wa Liverpool Andy Robertson anasema ni matumaini yake kwamba mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 33, raia wa Argentina hatasajiliwa na timu nyingine ya Ligi Kuu ya England.

**SMALLINGI KUBAKI ROMA**
MLINZI wa Manchester United, Chris Smalling mwenye umri wa miaka 30, anaonekana kuwa tayari kujiunga na AS Roma kwa mkataba wa kudumu. ***(Mirror)***

**NAPOLI WAMTAKA SOKRATIS**
RAIS wa Napoli, Aurelio de Laurentiis amesema wanataka kumsajili mlinzi wa Arsenal, Sokratis Papastathopoulos mwenye umri wa miaka 32 raia wa Ugiriki, hatua ambayo inaweza kutoa mwanya kwa Kalidou Koulibaly mwenye miaka 29, kujiunga na Manchester City. ***(Standard)***

**UNITED BADO NA SANCHO**
MANCHESTER United inajaribu kumaliza suala la mshahara ili kukamilisha uhamisho wa winga wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 20. ***(Star)***

**SEVILLA KUMBAKISHA REGUILON**
SEVILLA ina matumaini ya kuendelea kuwa na beki wa Real Madrid, Sergio Reguilon, 23, anayecheza kwa mkopo hapo kwa msimu mwingine. ***(Marca)***

**LIVER KUTOMUACHIA WILSON**
LIVERPOOL haitakubali kiungo wa kati, Harry Wilson mwenye umri wa miaka 23, kuondoka tena kwa mkopo licha ya Newcastle, Leeds na Southampton kuonyesha nia ya kumuwania.

**CHELSEA, MENDY HAKIELEWEKI**
CHELSEA imearifiwa kwamba lazima ilipe pauni milioni 30 ili kumsajili mlinda mlango wa Senegal, Edouard Mendy mwenye umri wa miaka 28, kutoka Rennes. ***(Telegraph)***

**ARSENAL YAMTAKA FELIPE**
ARSENAL inafikiria kumsajili kiungo wa kati wa West Ham na timu ya Taifa ya Brazil, Felipe mwenye umri wa miaka 27. ***(Football Insider)***

**BILLONG AWANIWA EPL**
KLABU za Crystal Palace, West Ham, West Brom, Norwich na Watford zinamnyatia mlinzi wa Ufaransa, Jean-Claude Billong mwenye umri wa miaka 26, anayecheza katika ligi ya Serie B katika klabu ya Salernitana. ***(Teamtalk)***

**ROMA YAMUWANIA PIATEK**
AS Roma inafikiria kumchukua mshambuliaji wa Hertha Berlin na Poland, Krzyszt Piatek, ili kuchukua nafasi ya Edin Dzeko. ***(Gazzetta dello Sport)***



HABARI MICHEZO

# PACHA WA SAMATTA ATUA COASTAL UNION

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA aliyecheza na Mbwana Samatta klabu ya African Lyon, Yusuph Soka, amejiunga na Coastal Union ya Tanga akitokea nchini Sweden alikokuwa akicheza soka la kulipwa.

Kocha Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda amesema mmoja wa wachezaji aliowaongeza kwa msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2020/21 unaotarajiwa kuanza kesho Jumapili, ni Yusuph Soka, straika mkongwe ambaye alikuwa akiichezea klabu ya AFC Eskilstuna iliyopo Ligi Daraja la Nne nchini Sweden.

"Nimeondokewa na vijana wangu vipenzi, lakini nimejitahidi kuziba mapengo yao, nimemchukua Peter Mwangosi kutoka Lipuli, Martin kutoka Geita Gold na mbele kwenye ushambuliaji nimemrudisha Hafidh aliyekuwa Gwambina FC, nimemrudisha pia Adil Sultan na mchezaji mzoefu Yusuph Soka," alisema Mgunda.

Soka alicheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2009/10 akiwa na Samatta, wakicheza kama pacha kwenye klabu ya African Lyon.

Ni msimu ambao Samatta alimaliza ligi akiwa na mabao sita, huku Soka akiwa amefunga matano, kabla ya Samatta kuhamia Simba msimu uliofuata.

Baadaye mchezaji huyo aliondoka kwenda nje ya nchi kucheza soka la kulipwa, na sasa amerejea kuichezea klabu hiyo ya jijini Tanga.

Wachezaji aliokuwa akiwataja Mgunda ni Martin Kazila ambaye alikuwa akiichezea Geita Gold, na mwingine ni Fadhili Hamisi na Raizin Hafidh ambaye awali alikuwa Coastal Union, lakini msimu uliopita alipelekwa Gwambina kwa mkopo, kabla ya kuamua kumrudisha tena kwenye kikosi chake msimu huu.

Coastal imewapoteza wachezaji wake muhimu kama Bakari Mwamnyeto alikwenda Yanga, Ibrahim Ame aliyejiunga na Simba, na kipa Masoud Abdallah Dondola aliyehamia KMC.

NYOMI YA MWANA FA...



Msanii wa muziki wa kizazi kipya, Ally Kiba akifanya vitu vyake jukwaani wakati wa uzinduzi wa kampeni ya mgombe ubunge kwa tiketi ya CCM Jimbo la Muheza, Hamisi Mwinjuma maarufu Mwana FA, uliofanyika Uwanja wa Jitegemee Muheza juzi, jioni. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Malale atoa neno usajili Ligi Kuu Bara

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Polisi Tanzania, Hamsini Malale, amesema kutokana na namna timu zilivyosajili, wanatarajia kupata upinzani mkubwa huku msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2020/21, akipatikana bingwa bora zaidi ya uliopita.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Malale alisema ameangalia usajili wa timu zote ikiwamo zilizopanda msimu huu, hivyo anaamini kutakuwa na ushindani mkubwa kwenye ligi hiyo.

Alisema msimu huu utakuwa mgumu, hivyo timu kama Simba, Yanga na Azam wasitarajie kama watatangaza ubingwa wakiwa wamebakiza mechi saba mkononi.

"Huu ni msimu mgumu sana ambao tunatarajia kuuona, timu zimefanya usajili mzuri, nadhani sasa bingwa atajulikana mwishoni mwa msimu, pia waamuzi hatutarajii kuyaona ya msimu uliopita," alisema Malale.

Alisema ana imani sekta ya waamuzi imefanyiwa kazi jambo ambalo anatarajia kuona wakifanya kazi yao kwa weledi na kuchezesha kwa kufuata sheria 17 za soka.

Kuhusu maandalizi ya mchezo wao dhidi ya Azam FC ,watakaocheza Jumatatu Septemba 7, Malale alisema kikosi chake kipo tayari kwa ajili ya kutafuta alama muhimu katika mechi hiyo.

"Tumejipanga, vijana wangu wana ari ya kufanya vizuri, muda tunacheza usiku, hivyo haitakuwa kigezo kwetu kupoteza pointi, tunawaheshimu Azam wamefanya usajili mzuri lakini hata sisi tumeboresha timu yetu," alisema Malale.

Polisi Tanzania watashuka dimbani Jumatatu ijayo wakiwa ugenini dhidi ya Azam FC, mchezo utakaopigwa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam.

## ZFF yaishusha Maji Makali

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Maji Makali inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Pemba katika msimu wa 2019/20 unaoendelea kwa sasa, imeshushwa madaraja mawili baada ya kushindwa kutokea uwanjani katika mechi tatu mfululizo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Msaidizi wa Kamati ya Mashindano ya Shirikisho la Soka Zanzibar Ofisi ya Pemba, Khamis Hamad, alisema kamati imechukua hatua hiyo kwa mujibu wa Kanuni ya Mashindano ya ZFF msimu wa 2019/20.

Alisema kwa mujibu wa kanuni hiyo, Sura ya 21 kifungu cha 1a (iv) kimeeleza wazi kuwa timu ambayo itafikisha mechi tatu mfululizo bila kutokea uwanjani itakuwa imejiondoa yenyewe katika mashindano na kushushwa chini madaraja mawili.

Aidha, alisema kwa mujibu wa kifungu hicho, timu hiyo kwa msimu wa 2020/21 itacheza Ligi Daraja la Pili Wilaya ya Michweni inapotokea.

"Timu ya Maji Makali kabla ligi kusimama kipindi cha mlipuko wa corona ilikuwa imefanya kosa hilo mara mbili, lakini baada ya ligi kuendelea imefanya kosa hilo tena na kufikisha michezo mitatu. Naomba timu zijue wajibu wake ikiwamo kufuata ratiba, tunajua timu zote zimeyumba kiuchumi lakini ni muhimu kufata ratiba," alisisitiza.

## Mundu yatupia jicho Daraja la Kwanza

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Mundu iliyoshuka daraja msimu uliomalizika wa 2019/20, imesema itajipanga ili kuhakikisha inarudi tena kucheza Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja msimu ujao wa ligi hiyo.

**Mundu ni miongoni mwa timu nne zilizoshuka daraja Kanda ya Unguja msimu huu wa 2019/20 hadi Ligi Daraja la Pili Mkoa kuelekea msimu wa 2020/21.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa timu hiyo, Malik Diku, alisema timu yake inatarajia kusajili wachezaji watakaoleta ushindani ambao unaweza kuwarudisha Daraja la Kwanza kwa mara nyingine.

Alisema anafahamu ugumu uliopo wa kupanda daraja, hivyo uongozi wa timu hiyo umedhamiria kuhakikisha unasajili wachezaji wazuri lengo kubwa likiwa ni kuipandisha timu yenye makazi yake Mkoa wa Kaskazini Unguja.

"Tumeshuka msimu huu, lakini lengo letu ni kurudi tena na kucheza Ligi Daraja la Kwanza Kanda kwa msimu ujao, mwaka huu hatukujipanga vema ndio maana tumeshuka na tumeona kosa letu lilikuwa wapi, hivyo makosa yote ya msimu huu uliyoisha tutayafanyia kazi msimu ujao," alisema.

# Michezo

Jumamosi Septemba 5, 2020

Nipashe




ARTETA AHESABU SIKU AUBAMEYANG KUSAINI HABARI UK 22

SHUTI...




Winga wa Ujerumani, Leroy Sane akimjaribu kwa shuti hafifu kipa wa Hispania, David De Gea katikati ya walinzi wa timu hiyo kwenye mechi ya Ligi ya Mataifa ya Ulaya iliyopigwa juzi usiku katika Uwanja wa Mercedes-Benz-Arena jijini Stuttgart, Ujerumani na kumalizika kwa sare ya bao 1-1. Mabao yalifungwa na Jose Luis Gaya kwa Hispania na la Ujerumani likizamishwa nyavuni na Timo Werner. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA YATOA SABABU KUVUNA 3 ZA PRISONS

●●● Mwambusi amwekea Zlatko mbinu za Mayanga mezani, huku akieleza tayari...

**Na Saada Akida**

LICHA ya kuchelewa kujiunga na timu yake huku kikosi chake kikiundwa na nyota wengi wapya, Kocha Mkuu wa Yanga, Mserbia Zlatko Krmpotic, amepewa mbinu zote na msaidizi wake, Juma Mwambusi, zitakazoiwezesha timu hiyo kuibuka na pointi tatu dhidi ya wapinzania wao, Tanzania Prisons kesho.

Yanga itaikaribisha Prisons katika mechi yao ya ufunguzi wa Ligi Kuu Bara itakayopigwa Uwanja wa Mkapa jijini Dar es Salaam kesho majira ya saa 1:00 usiku.

Mchezo huo utakuwa wa kwanza kwa Zlatko kuiongoza Yanga ikiwa ni wiki moja tangu ajiunge na timu hiyo, lakini Mwambusi ambaye naye alijiunga na klabu hiyo siku nne kabla ya Mseribia huyo kutua, amesema anamfahamu vema Kocha wa Prisons, Salum Mayanga tangu akiwa na Ruvu Shooting msimu uliopita, hivyo hiyo haiwezi kuwa sababu kwao ya kushindwa kuibuka na ushindi.

Mwambusi amesema licha ya kufahamu uwezo wa Mayanga ambaye naye ameanza kuinoa Prisons msimu huu, watashuka dimbani kwa tahadhari kubwa na kwenda kutafuta matokeo.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mwambusi alisema wamejipanga kuhakikisha wanapata alama tatu katika mchezo huo, licha ya kwamba kikosi chao kinaundwa na nyota wengi wapya.

Alisema msimu huu ligi itakuwa na ushindani mkubwa, lakini watahakikisha wanakuwa makini katika maandalizi yao pamoja na kufuatilia mbinu na mfumo wa kila mpinzani wanayekutana naye.

"Kwa sasa Prisons inanolewa na kocha mwingine, ambaye namfahamu uwezo wake na ninamheshimu, amefanikiwa kufundisha timu mbalimbali na kufanya vizuri, tutaingia uwanjani kwa tahadhari kwa lengo moja tu la kutafuta matokeo.

"Kwa sasa nashirikia na Kocha Mkuu, Zlatko kufuatilia mbinu na mifumo yake hasa kwa msimu uliopita kwa timu aliyoifundisha wakati anacheza na timu kubwa," alisema Mwambusi, ambaye hii ni mara ya pili kuwa kocha msaidizi wa timu hiyo baada ya awali kufanya kazi na Mholanzi Hans van der Pluijm.

Alisema kwa upande wa wachezaji wapo tayari kwa ushindani na wanahitaji ushindi ili kupata pointi tatu.

"Kikubwa mashabiki wajitokeze kwa wingi kutupa sapoti, kwa asilimia kubwa tumefanikisha maandalizi ya mwisho kwa umakini kabisa," alisema Mwambusi. Yanga ambayo msimu uliopita ilimaliza nafasi ya pili nyuma ya mabingwa, Simba, kwa sasa imeweka kambi Kigamboni nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam kwa ajili ya msimu huu wa 2020/21 unaoanza kesho kwa mechi sita kupigwa.

Mbali na mechi hiyo, kwa kesho majira ya saa 10:00 alasiri, mabingwa watetezi wa ligi hiyo, Simba watakuwa wageni wa Ihefu FC katika Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, Mtibwa Sugar ikiwa mwenyeji wa Ruvu Shooting katika Uwanja wa CCM Gairo.

Mechi zingine zitakazopigwa kesho itakuwa kati ya Namungo FC ambayo itaialika Coastal Union kwenye Uwanja wa Majaliwa mkoani Lindi huku Biashara United ikiwa mwenyeji wa Gwambina FC katika dimba la Kumbukumbu ya Karume mjini Musoma wakati Dodoma Jiji ikishuka katika uwanja wake wa nyumbani wa Jamhuri mjini Dodoma kuikaribisha Mwadui FC.

Raundi ya kwanza itakamilika keshokutwa Jumatatu kwa KMC FC kuikaribisha Mbeya City Uwanja wa Uhuru, huku Kagera Sugar ikiwa katika dimba la Kaitaba mjini Bukoba kuialika JKT Tanzania wakati huo Azam FC ikiwa mwenyeji wa Polisi Tanzania, Uwanja wa Chamazi.

# BWALYA AANIKA DENI LAKE SIMBA

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Simba ikitarajia kushuka Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya kesho kuivaa Ihefu FC kwenye mechi ya ufunguzi wa Ligi Kuu Bara, Kiungo mpya wa klabu hiyo, Mzambia Rally Bwalya, amesema anajiona ni mwenye deni kubwa kila anaposhuka dimbani kutokana na imani kubwa kwake waliyonayo mashabiki wa klabu hiyo.

Bwalya ambaye amejiunga na Simba akitokea Lusaka Dynamos ya Zambia ni miongoni mwa nyota wa kigeni wanne waliosajiliwa na klabu hiyo msimu huu, wengine wakiwa ni mshambuliaji Mkongomani Chris Mugalu waliyetokana naye timu moja, Mkenya Joash Onyango aliyemaliza mkataba na Gor Mahia ya Kenya na Mghana Bernard Morrison mchezaji huru baada ya kumalizana na Yanga.

Lakini Bwalya ambaye amekuwa kipenzi cha mashabiki wa timu hiyo,

kuelekea mchezo wa kwanza wa ligi dhidi ya Ihefu, amesema akipata nafasi ya kucheza atajituma ili kushirikiana vema na wenzake kuipa timu ushindi.

**"Kila ninapoingia uwanjani najiona nina deni kubwa kwa sababu Wanasimba wana imani kubwa na mimi, siwezi kuwaangusha nitahakikisha najituma kwa kila hali ili kuwafurahisha," alisema akiiambia tovuti ya klabu hiyo.**

Katika mchezo wa kirafiki Simba iliyocheza dhidi ya Arusha FC Jumatatu wiki hii katika Uwanja wa Sheik Amri Abeid na kuibuka na ushindi wa mabao 6-0, Bwalya alifunga bao moja.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >